# Nipashe

Jumatano Novemba 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580403

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




siasa

Uhasama majimboni, 'miba njiani', corona vibano vilivyokwaza kinamama Zanzibar

Ni dhana inayowahusu wote waliopigiwa na wapigakura

KILIO RUZUKU

Ajabu vyama bila vigezo kulilia huruma ya serikali

UKURASA 11

**WANAFUNZI** 5,100 zaidi elimu ya juu wapatiwa mikopo

UKURASA 3



**MPANGO** awawashia moto watumishi Wizara ya Fedha

UKURASA 3

# Saruji sasa kaa la moto

**MA-RC** waanza kutekeleza agizo la PM, Ma-DC nao wajitosa, maeneo mengine yaadimika ...*Endelea Uk. 2*



Wakazi wa eneo la Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam, wakiangalia sehemu ya nyumba yao, iliyobomolewa na mvua iliyonyesha jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwili askari aliyeuawa wakutwa umefukiwa

UKURASA 17

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**KIGOGO MWANDAMIZI POLISI AFARIKI DUNIA**

NAIBU Kamishna wa Fedha na Lojistiki wa Jeshi la Polisi, Dhahiri Kidavashari (56), amefariki dunia katika Hospitali ya...

UKURASA WA 4

**WAKUTWA WAMEKUFA KANDO YA BARABARA**

WATU wawili wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 20 na 25 wamekutwa wamekufa na miili yao kutelekezwa pembeni mwa njia katika....

UKURASA WA 5

**MKURUGENZI JAMII MEDIA AHUKUMIWA KIFUNGO CHA NJE**

MKURUGENZI Mtendaji wa Jamii Media, Maxence Melo, amehukumiwa kutumikia kifungo cha nje baada...

## TMA yatabiri mvua kubwa kunyesha

UKURASA 2

**MICHEZO** **MASTRAIKA WA PLATEAU WAITISHA SIMBA CAF** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK. 6



Vyombo vya moto vikipita kwa shida katika Barabara ya Salasala Tangi la DAWASA, iliyofurika maji kutokana na mvua iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SALOME KITOMARI**

# Saruji sasa kaa la moto

**Na Waandishi Wetu**

NI kaa la moto. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na mambo yanavyoendelea kila kona kuhusu bei ya saruji pamoja na kuadimika kwa bidhaa hiyo katika baadhi ya maeneo nchini.

Hali piyo pia inatokana na kuibuka kwa mambo mapya katika utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la kuwataka wakuu wa mikoa kufuatilia kiini cha tatizo la kupanda kwa bei pamoja na kuwapo kwa uhaba wa bidhaa hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, na wakuu wa wilaya, jana walilazimika kufanya ziara katika maduka na kuona hali halisi, huku wengine wa wilaya wakijitosa kuwasaidia mabosi wao katika kukabiliana na hali hiyo.

Mongela jana alikutana na baadhi ya wasambazaji wa saruji mikoa ya Kanda ya Ziwa na kumweleza kuwa kuna uhaba wa bidhaa hiyo katika viwanda.

Jonex Joel, msambazaji wa saruji, alimweleza Mongela kuwa awali alikuwa akipata tani 15,000 kwa mwezi, lakini sasa anakosa na kuambulia tani 7,000 kwa mwezi.

Joel, ambaye ni Wakala wa Twiga Cement, alisema soko la saruji ni kubwa, lakini haipatikani kwa kiwango wanachotaka ili kutosheleza mahitaji ya soko na kuongeza kuwa kila akiagiza anapewa nusu ya kiasi alichoagiza na kwamba wauzaji wa rejareja hawapaswi kuuza mfuko kwa Sh. 23,000.

Alisema kwa sasa mfuko mmoja wanauza Sh.18,500 hadi 19,000 kwa bei ya jumla, lakini anashangaa kwa bei ya rejareja ikiuzwa Sh. 23,000.

Msambazaji mwingine, Pravin Shah, wakala wa Dangote, alisema hajapandisha bei ya saruji licha ya kusikia mtaani imepanda na kuongeza kuwa anauza mfuko mmoja kwa Sh. 18,500 hadi Sh. 19,000.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea, maghala ya kuhifadhia bidhaa hiyo, Mongela aliwaonywa wauzaji wadogo kuacha kupandisha bei kwa kuwa haijapanda kwa wauzaji wa jumla.

**MA-DC WAINGIA KAZINI**

Baadhi ya wakuu wa wilaya wameanza kufanya ukaguzi kwa mawakala na maduka ya kuuzia saruji ili kuhakikisha inapatikana.

Viongozi hao na wilaya zao kwenye mabano ambao walizungumza na Nipashe kwa simu ni Daniel Chongolo (Kinondoni), Frank Mwaisumbe (Longido), Dk. Chelesitino Mofuga (Mbulu ), Asia Abadallah (Kilolo) na Rashid Mwaimu (Kyerwa). Walisema wameamua kuingia kazini kuhakikisha wanachunguza na kuchukua hatua dhidi ya wote waliohusika na upandishaji holela wa bei.

Chongolo alisema wameanza kuchukua hatua ikiwamo kutembelea maduka na viwanda na kwamba kazi kubwa kwa sasa ni kutafuta sababu ya kuadimika kwa bidhaa hiyo kwa kuwa katika uchunguzi wao walikuta stoo 17 hazina bidhaa na kwamba walibaini, pia inapopatikana inauzwa kati ya Sh. 17,000 hadi 22,000 wilayani humo ambako kuna kiwanda cha Twiga.

“Nilikwenda kiwandani na kukuta mfuko unauzwa Sh. 13,500 hadi 14,500 na ni bei za tangu Mei ila mtaani imepanda ila walijiuliza zaidi nini kimesababisha bei kuwa juu na saruji kupotea ndipo kazi zaidi ilipoanza,” alisema.

Alisema wamebaini baadhi ya wafanyabiashara wa kati kwa kushirikiana na madalali, wanatengeneza hali hiyo ya uhaba wa saruji kwa kununua saruji ya kutosha na kuhifadhi ili kuongeza bei.

Kutokana na uchunguzi huo, kuna wafanyabiashara sita wanachunguzwa kwa tuhuma za kupandisha bei na uchunguzi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Novemba 9, mwaka huu, Nipashe iliibua suala la uhaba wa saruji nchini, na kubaini kuwa maneno mengi ilipanda kwa ongezeko la Sh. 3,000 hadi 8,000, huku baadhi ya maeneo ikiadimika kabisa.

Mofuga alisema kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ilifanya ukaguzi na kutoa maagizo ya kutopandisha bei na kwamba anafuatilia kwa karibu iuzwe kwa Sh. 16,000. Alisema saruji wilayani humo inauzwa kati ya Sh. 17,000 na 18,000 japo bei elekezi ni Sh. 16,000.

Naye Mwaisumbe alisema wamefuatilia kwa karibu na kubaini ilipanda hadi kufikia Sh. 17,000 ila kwa sasa bei imeanza kushuka hadi kufikia Sh. 15,500 na bado wanaendelea kufuatilia zaidi kujua bei halisi ambayo mlaji anapaswa kununua.

Alisema Longido haina kiwanda cha saruji na wanategemea kutoka Arusha na Tanga na kwamba kupanda kwa bei kumeathiri shughuli nyingi za ujenzi.

Mwaimu kwa upande wake alisema hali ya upatikanaji wa saruji ni nzuri na bei si ya kutisha kulinganisha na jiografia ya wilayani humo ambayo ni Sh. 22,000 na kwamba kwa sasa inauzwa kati ya Sh. 23000 na 25,000.

Abdallah kwa upande wake alisema wilayani Kilolo wametembelea maduka ya saruji na kujua bei ya saruji na upatikanaji wake na kubainisha kuwa upatikanaji wake ni mkubwa na inauzwa kwa Sh. 19,000.

***Imeandikwa na Richard Makore (MWANZA) na Francis Godwin, (IRINGA)***

# Kigogo polisi afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Kamishna wa Fedha na Lojistiki wa Jeshi la Polisi, Dhahiri Kidavashari (56), amefariki dunia.

Kadavshari ambaye alikuwa Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), alifariki jana katika Hospitali ya Christian Medical Center Trust (DCMCT) jijini Dodoma.

Katika enzi za uhai wake amewahi kuwa Kamanda wa Polisi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mbeya na Katavi.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Simon Sirro, alitangaza kifo cha ofisi huyo mkuu.

“Ninasikitika kutangaza kifo cha Naibu Kamishna wa Polisi, Dhahiri Kidavashari, kilichotokea leo (jana) katika hospitali hiyo wakati akiendelea kupatiwa matibabu,” alisema.

IGP Sirro alisema taratibu za mazishi zinaendelea kwa kushirikiana na familia ya marehemu na kwamba msiba uko Kisasa, nyumba mia tatu jijini Dodoma.

Mwaka 2015 alikuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi na mwaka 2017 alihamishwa kwenda kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya.

Julai, 2017 IGP Sirro alimhamishia DCP Kidavashari Makao Makuu ya Upelelezi akitokea Mbeya.

**“Ninasikitika kutangaza kifo cha Naibu Kamishna wa Polisi, Dhahiri Kidavashari, kilichotokea leo (jana) katika hospitali hiyo wakati akiendelea kupatiwa matibabu,” alisema.**

# TMA yatabiri mvua kubwa kunyesha

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema mvua kubwa inatarajiwa kunyesha katika baadhi ya maeneo ya nchini ikiwamo mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora, Rukwa, Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe.

Hayo yalibainishwa jana kwenye tovuti ya TMA, ikielezea kuhusu utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24.

Pia utabiri huo ulionyesha, Mkoa wa Dar es Salaam utaendelea kupata mvua nyepesi na ngurumo hadi Novemba 21, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa TMA, Dk. Hamza Kabelwa, aliiambia NIPASHE juzi kuwa:

“Sasa hivi ni msimu wa mvua kwa utabiri zinaonekana hadi Novemba 21 kwa Dar es Salaam, ingawa kunakuwa na mabadiliko ya utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24, yanatarajiwa mabadiliko.”

Dk. Kabelwa alisema maeneo ambayo yanapata mvua za msimu mmoja na misimu miwili kwa mwaka ambayo yapo Kaskazini mwa nchi, ukanda wa Ziwa Victoria, Arusha, Kilimanjaro na Manyara, Tanga, Pemba, Unguja, na Dar es Salaam zitaendelea hadi Desemba.

Alisema pia Januari inatarajiwa kuendelea kuwa na mvua, na kwamba Tabora, Dodoma, Kigoma, Katavi, Njombe, Rukwa na Mbeya zilianza kunyesha mwezi huu hadi Aprili mwakani.

“Wiki ya pili maeneo mengi nchini inanyesha mvua, hata ambayo inayopata mvua kwa misimu miwili kuna mvua ya vuli inaendelea kunyesha.

Kwa mujibu wa Dk. Kubelwa, Jangwani kujaa ni matokeo ya mvua inayonyesha kwingine na kutiririsha maji Mkoa wa Dar es Salaam.

**FOLENI JIJINI**

Kaimu Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camillius Wambura, akizungumza na Nipashe juzi, alisema hali ya mvua inayoendelea kunyesha, imeleta adha ya foleni hususani maeneo ya mjini.

Alisema ingawa hapakuwapo na taarifa za athari za moja kwa moja, kulikuwapo na msongamano wa magari.

“Jangwani pamejaa maji, shida kubwa ni foleni ambayo ipo kwenye maeneo mengi ya mji, athari ni hiyo,” alisema Wambura.

## HABARI KITAIFA

# Mpango awawashia moto watumishi Wizara Fedha



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (kulia), akipokelewa kwa furaha na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Doto James, baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara zilizopo Mtumba, jijini Dodoma juzi. **PICHA: WFM**

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, jana alikutana na watumishi wa wizara hiyo, kwa mara ya kwanza tangu alipoapishwa juzi huku akiwataka kufanya kazi kwa bidii.

Katika kufanya hivyo, aliwataka kusimamia kikamilifu mapato na matumizi ya fedha za umma, ili kufanikisha malengo ya maendeleo yaliyotolewa na Rais John Magufuli, wakati akizindua Bunge la 12 wiki iliyopita mjini hapa.

Dk. Mpango juzi aliapishwa kushika wadhifa huo kwa mara nyingine baada ya kuteuliwa na Rais. Alikuwa waziri katika wizara hiyo kwa miaka mitano iliyopita.

Mpango alisema bado kuna shida kubwa katika eneo la matumizi ya fedha za umma, kwa kuwa fedha zinazopelekwa kutekeleza miradi mbalimbali hazitumiwi vizuri na kusababisha baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

"Tunahitaji jicho la pekee. Katika halmashauri tunapeleka fedha za miradi, lakini mimi nakadiria kuna upotevu wa takribani asilimia arobaini ya fedha hizo kwa hiyo ni lazima tuwe na jicho kali, ili kuokoa fedha za wananchi," alisema.

Waziri Mpango alisema mpango wa kununua ndege, meli na vitu vingine katika kipindi cha miaka mitano, itafanikiwa iwapo kila mmoja katika nafasi yake atasimama imara kuhakikisha mapato yanakusanywa na kutumika kikamilifu.

Alisema Watanzania wana matarajio makubwa kutoka katika serikali yao, hivyo watumishi wa wizara ambao ni kitovu cha maendeleo, wanatakiwa kuhakikisha matarajio hayo yanafikiwa.

Dk. Mpango aliwashukuru watumishi wa wizara yake kwa utendaji kazi mzuri kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita lakini akaomba waongeze jitihada na maarifa katika kutekeleza miongozo mbalimbali ikiwamo hotuba ya Rais ya Kufungua Bunge la 12, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuweka mikakati madhubuti ya kufanikisha utekelezaji wake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alimhakikishia Waziri Mpango kwamba menejimenti imejipanga kikamilifu kuhakikisha inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu ili nchi ifikie malengo iliyojiwekea katika kukuza uchumi.

# Wanafunzi 5,100 wapewa mikopo bil.20/-

**Na Mwandishi Wetu**

**"Tuna wanafunzi wachache ambao maombi yao yana upungufu ambao kuanzia kesho (leo) wataingia katika akaunti zao za SIPA walizotumia kuomba mkopo na kurekebisha kwa kuweka nyaraka sahihi na tutazifanyia uchambuzi na wenye sifa watapangiwa mikopo mapema iwezekanavyo," alisema Badru.**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza orodha ya wanafunzi 5,168 wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo kwa awamu ya pili yenye thamani ya Sh. bilioni 19.9.

Wakati bodi hiyo ikitangaza orodha ya wanufaika wa awamu ya pili, pia imesema wanafunzi waliokosea katika ujazaji fomu za maombi, sasa wanaruhusiwa kufanya marekebisho.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, ilisema jumla ya wanafunzi 52,473 wa mwaka wa kwanza wamepangiwa mkopo yenye thamani ya Sh. Bilioni 170.02.

Badru alisema Novemba 11, mwaka huu, HESLB ilitangaza orodha ya awamu ya kwanza ya wanafunzi waliopangwa mikopo iliyokuwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza 47,305 ambao walipangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. Bilioni 150.03.

"Wanachotakiwa kufanya kwa sasa ni kutembelea katika akaunti zao za SIPA walizotumia kuomba mkopo na watapata taarifa za kina kuhusu mkopo," alisema Badru katika taarifa yake hiyo,

Katika hatua nyingine, Badru alisema waombaji ambao maombi yao yalikuwa na upungufu, HESLB imetoa siku tano kuanzia leo kurekebisha taarifa zao na kuzituma kwa njia ya mtandao.

"Tuna wanafunzi wachache ambao maombi yao yana upungufu ambao kuanzia kesho (leo) wataingia katika akaunti zao za SIPA walizotumia kuomba mkopo na kurekebisha kwa kuweka nyaraka sahihi na tutazifanyia uchambuzi na wenye sifa watapangiwa mikopo mapema iwezekanavyo," alisema Badru.

Katika mwaka wa masomo wa 2020/21, serikali imetenga Sh bilioni 464 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi 145,000 wa elimu ya juu wakiwemo 54,000 wa mwaka wa kwanza na 91,000 wanaoendelea na masomo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO** ....13........ **YA 20**.20.......

..M.M. INDUSTRIES LTD.............. **MDAI**

**DHIDI YA**

ELCAT BUILDERS (T) LTD.............. **MDAIWA**

**KWA:** ELCAT BUILDERS (T) LTD
**DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe ...30/11/2020..... Saa **7.00** Mchana. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusomwa hukumu ya shauri hilo

**ANGALIA:**
Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea Kuitwa Shaurini, itaweza kusikiliza bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe ....16.... Mwezi wa ...November........, **2020.**

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU - DAR ES SALAAM**

216003102

# Wakutwa wamekufa kando ya barabara

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

WATU wawili wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 20 na 25 wamekutwa wamekufa na miili yao kutelekezwa pembeni mwa njia katika kijiji cha Mkowela, Tunduru mkoani Ruvuma.

Mashuhuda wa tukio hilo, walisema juzi kuwa wakazi wa kijiji hicho walishindwa kuitambua miili hiyo na kutoa taarifa Polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi na hatimaye kuihifadhi kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

Diwani mteule wa Kata ya Namakambale, Mfaume Wadali, alisema miili hiyo iligunduliwa Novemba 14, mwaka huu na kijana wa kifugaji ambaye aliiona baada ya kupita eneo hilo kwa ajili ya kuokota embe.

Wadali alisema baada ya tukio hilo, kijana huyo alikwenda kutoa taarifa kijijini kisha yeye, viongozi wa kijiji na baadhi ya wazee maarufu walikwenda katika eneo la tukio na kukuta mwili wa kwanza ukiwa umelala huku sura yake ikiwa imetazama chini.

Pia alisema walipotazama umbali wa mita 100, waliona mtu mwingine akiwa amelala pembeni ya barabara na walipokwenda kumtazama, walimkuta akiwa amefariki dunia.

Alisema baada ya kubaini hali hiyo, walitoa taarifa kituo kidogo cha Polisi Nakapanya na baadaye wakasambaza taarifa katika vijiji vilivyoko jirani na eneo hilo na wananchi wengi walijitokeza kuwatambua lakini hakuna hata mmoja aliyeonyesha kuwafahamu.

Kutokana na hatua hiyo, alisema polisi waliichukua miili hiyo na kuipeleka katika hospitali ya wilaya kuhifadhiwa na kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Diwani huyo alieleza kuwapo taarifa za makundi ya vijana kutoka wilaya jirani za Nanyumbu na Masasi mkoani Mtwara ambao wamekuwa wakidandia magari ya mizigo kwa ajili ya kuiba mizigo na kuishusha chini na kuruka na kwamba kama ndivyo huenda walishuka wakati gari likiwa limeshika kasi na kuanguka na kufariki kutokana na kukosa huduma muda mrefu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, pamoja na kuthibitisha tukio hilo alisema kuwa polisi wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha tukio na watu hao walitoka wapi na wafikaje katika eneo hilo.

Pia aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Tunduru ambao wamepotelewa na ndugu zao kwenda katika hospitali ya wilaya, ili kuwatambua na kuwasaidia polisi kubaini ukweli wa tukio hilo.



Sehemu ya wanachama wa muungano wa klabu za waandishi wa habari Tanzania (UTPC), wakifuatili hotuba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa UTPC, mjini Morogoro jana. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Wanahabari watakiwa kulinda taaluma, amani

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, amewataka wanahabari kulinda taaluma na kutekeleza wajibu wao katika kulinda amani ya nchi na kuwa chachu ya maendeleo.

Pia amewataka wamiliki wa magazeti kuwa na mikataba ya wafanyakazi wao wakati wa kuomba leseni za uendeshaji vinginevyo watakosa fursa hiyo.

Dk. Abbas ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali, alisema jana hayo wakati akifungua mkutano mkuu wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) mjini hapa.

Alisema Rais John Magufuli katika awamu ya tano muhula wa pili, ameahidi kuimarisha mazingira ya wanahabari ya kufanya kazi na kuwataka kujenga hoja juu ya mambo mahususi wanayoona serikali inapaswa kuyasimamia zaidi kwa maslahi yao.

"Waandishi wa habari tuendelee kuwa mawakala wa amani kwa namna yoyote kupitia kalamu zetu na vyombo vyetu vya habari. Zaidi tuepuke kutoa kipaumbele kwenye kila kinachozungumzwa na kila mtu na kukifanya kuwa ndiyo habari kubwa. Nchi haiwezi kuendelea kama hakuna amani na utulivu," alisisitiza.

Pia aliwahimiza waandishi wa habari kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kuepuka kuchangishana pale inapotokea mwandishi anaugua na kusisitiza UTPC kuangalia namna ya kuzisaidia klabu za waandishi wa habari kuwa na vyanzo vya uhakika vya kiuchumi ili kumudu maisha badala ya kuchangiana kwenye makundi ya kijamii panapotokea shida.

"Ifike hatua UTPC au klabu za waandishi wa habari kuanzisha SACCOS (Chama cha Akiba ya Kuweka na Kukopa). Bima ya afya pia ni jambo la kutilia mkazo zaidi ingawa zipo taarifa kuwa baadhi ya klabu zimeshaanza hili," alisema.

Kuhusu kiwango cha diploma kwa wanataaluma ya habari kwa mujibu wa sheria, Dk. Abbas alisema ifikapo Desemba Mosi, 2021, wale wanaoendelea na masomo ya uandishi wa habari wataendelea na kazi isipokuwa wale ambao watakuwa bado hawajaanza itakuwa mwisho.

Awali, akimkaribisha Dk. Abbas kufungua mkutano huo, Rais wa UTPC, Deogratius Nsokolo, alisema mwandishi wa habari si adui wa serikali kama inavyodhaniwa na kwamba uandishi ni taaluma kama ilivyo taaluma nyingine yoyote na si uanaharakati.

# Wanachama CCM warudisha kadi kisa mgombea udiwani kushindwa

**Na Anthony Kayanda, KIGOMA**

BAADHI ya wanachama 1,100 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Kata ya Mwakizega, Uvinza mkoani Kigoma, wamerudisha kadi zao za uanachama na kuzikabidhi kwa Katibu wa Kata hiyo.

Wakizungumza jana na mwandishi wa habari hii, wanachama hao walisema wamefanya hivyo baada ya kutoridhishwa na matokeo ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, baada ya mgombea udiwani wa CCM kushindwa.

Mwamvua Mwakatika, mmoja wa wanachama hao, alisema kulikuwa na hujuma zilizosababisha mgombea wa CCM, Swabiru Musa kushindwa, hivyo wanachama wamekerwa baada ya kuona viongozi wamepuuza malalamiko yao.

"Tumewaeleza viongozi wetu wa kata ili wafuatilie suala hili, lakini hadi sasa wapo kimya. Hii ina maana wameridhika na hizi hujuma, sasa tumeamua kurudisha kadi zetu za uanachama ofisini (ngazi ya kata) kwa sababu chama hakioni umuhimu wetu," alisema Mwamvua.

Naye Hafsa Ramadhani alisema kitendo cha mgombea udiwani wa CCM kufanyiwa mizengwe ili ashindwe kimewaudhi wengi ndiyo maana wameamua kurudisha kadi zao kwa hiari.

Alisema kwa sasa hawako tayari kuona haki yao inaporwa kwa sababu ya chuki binafsi za baadhi ya wanachama wenzao kutokana na kushindwa kwenye kura za maoni, hatimaye wakaungana na wapinzani kumhujumu mgombea wa CCM.

Juma Yassin wa Mwakizega, alisema ameamua kurudisha kadi yake kwa katibu wa CCM kata, ili kuonyesha hasira zake kwa viongozi wa chama baada ya kushindwa kupigania haki ya mgombea wao.

"Mgombea wetu (Swabiru Musa) aliibiwa kura makusudi kwani kuna ushahidi wa wazi kabisa. Baadhi ya vituo taa zilizimwa makusudi, vituo vingine matokeo yalibadilishwa na kumpa ushindi mgombea wa DP, hili jambo halikubaliki," alisema Yassin.

Katibu wa CCM Kata ya Mwakizega, Mbano Gwemela, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo ambapo hadi sasa kadi 1,100 zimerejeshwa ofisini kwake.

"Hapa nilipo kuna kadi 360 kutoka kijiji cha Katete na kadi 740 zinatoka kijiji cha Mwakizega. Kwa kweli jambo hili linanipa wakati mgumu sana kukabiliana nalo na wanachama hawataki kuelewa lolote kwa sababu bado wana hasira," alisema Gwemela.

Alisema wanacholalamikia wanachama hao ni kile kinachodaiwa kuwa mgombea wa CCM alishinda uchaguzi, lakini akatangazwa mgombea wa chama cha DP, Patrick Bitaliho.

Wanaorudisha kadi kwa wingi ni vijana na wanawake ingawa kuna baadhi ya wazee pia wamerudisha kadi.

"Kadi zote nilizopokea nimezitunza ofisini hadi hapo sakata hili litakapomalizika maana wanachama wanaonekana kupata jazba, lakini bila shaka hasira ikipoa watarudi kuchukua kadi zao," alisema.

Wanachama hao wanataka uchaguzi huo urudiwe kwa vile haukuwa huru na haki, jambo lililopelekea mgombea wao kudhulumiwa ushindi.

Kwa upande wake Swabiru alikataa kuzungumzia sakata hilo ingawa alisema anakusudia kukata rufani kupinga matokeo yaliyomnyima ushindi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kigoma, Amandus Nzamba, alipotafutwa kuzungumzia sakata hilo akisema kuwa hajapata taarifa yoyote, lakini akasema chama kina utaratibu wake wa kupokea na kusikiliza malalamiko ya wanachama.

"Kitendo cha wanachama kurudisha kadi ofisi ya kata si suluhisho la tatizo kama lipo. Kama kuna jambo lolote lililowakera walipaswa kulitatua kwa kufuata katiba na kanuni za chama ambazo ziko wazi," alisema Nzamba.

# Mkurugenzi wa Jamii Media ahukumiwa kifungo cha nje

**Hellen Mwango na Antony Benedictor**

MKURUGENZI Mtendaji wa Jamii Media, Maxence Melo, amehukumiwa kutumikia kifungo cha nje baada ya kukutwa na hatia kwa kosa la kuzuia askari kutekeleza majukumu yao ikiwamo sharti la kutokurudia kosa hilo ndani ya mwaka mmoja.

Hukumu hiyo ilisomwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Hata hivyo, mahakama hiyo imemwachia huru mshtakiwa wa pili, Mike Mushi baada ya kukuta hana hatia katika makosa yote yaliyokuwa yakiwakabili.

Hakimu alisema Mushi alikuwa ni kama msindikizaji katika kesi hiyo na kwamba hakuna ushahidi uliomgusa kutoka upande wa Jamhuri.

Aidha, upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliita mashahidi sita, utetezi mashahidi wawili washtakiwa wenyewe.

Awali, kabla ya kusomwa hukumu hiyo Wakili wa Serikali, Faraji Ngukah aliomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa kwa kuwa kitendo alichokifanya cha kuzuia askari kutekeleza majukumu yao ni hatari kwa taifa.

Akiwasilisha hoja za kuomba nafuu ya mahakama, Wakili wa Utetezi, Bernedict Ishabakaki, alidai kuwa sheria iliyotumika katika kosa hilo ina adhabu mbadala ikiwamo faini, mahakama imemuhukumu kutoa faini kwa kuwa ameajiri vijana wanaomtegemea, hivyo faini itakuwa fundisho.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, Hakimu Shaidi alisema mshtakiwa alionekana kuwa na makosa katika kesi ambazo zilifunguliwa awali zote zikiwa na makosa yanayofanana.

Alisema Jeshi la Polisi liko kwa ajili ya Watanzania wote kazi yake ni kupeleleza na wajibu wa kila mwananchi kushirikiana nalo na mahakama inakukumbusha hilo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Melo na Mushi walidaiwa kuendesha mtandao ambao haujasajiliwa kwa kikoa (domain) cha .tz na katika shtaka jingine walidaiwa kuzuia askari polisi kutekeleza majukumu yao, makosa wanayodaiwa kuyatenda kati ya Desemba 9, 2011 na Desemba 13, 2016 katika eneo la Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jamii Forum, Maxence Melo, akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha mwaka mmoja nje na kutofanya kosa lolote kutokana na kesi iliyokuwa ikimkabili ya kuzuia Polisi kufanya kazi yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 29 mbaroni madai ya uhamiaji haramu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

IDARA ya Uhamiaji mkoani Dodoma, katika operesheni yake ya wiki moja na nusu, imekamata watu 29 kwa madai kuwa ni wahamiaji haramu, kutoka Ethiopia, Rwanda Uganda na Bangladesh, kwa kosa la kuingia nchini bila vibali.

Aidha, Watanzania watano wanashikiliwa na Idara ya hiyo Mkoa wa Dodoma, kwa kosa la kuwasafirisha wahamiaji hao kwa kutumia usafiri wa bodaboda na gari aina ya Fuso.

Ofisa Uhamiaji mkoa wa Dodoma, James Mwanjotile, alisema walikamatwa katika barabara kuu ya Iringa eneo la Mtera.

Alisema katika idadi hiyo, 15 ni Waethiopia, Wabangladesh wawili, Wanyarwanda 11 na mmoja ni kutoka Uganda.

Pia, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kutokana na Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Dodoma kushirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana kwa kutoa taarifa za uwapo wa wahamiaji haramu wanaowahisi wanapopita katika maeneo yao.

"Ni jambo la aibu Mtanzania kumsaidia kumsafirisha mhamijai haramu, suala la kulinda amani ya nchi yetu ni la kila mmoja wetu, hivyo wanaojihusisha na kusafirisha hawa watu waache mara moja," alisema Mwanjotile

Akizungumzia kuhusu Watanzania watano, waliokamatwa alisema kuwa walikamatwa wakiwa na wahamiaji hao wakiwasaidia kusafiri kutoka jijini Dodoma kwenda Makambako.

"Hawa bodaboda wote wawili tuliwakamata wakiwa na hawa Wahabeshi wakiwasafirisha kwa pikipiki kutoka Dodoma kuwapeleka Makambako pamoja na yule wa gari aina ya fuso ambaye alikuwa na wahamiaji haramu watatu kwenye gari," alisema.

## NMB sasa yazindua 'Mwanamke Jasiri'

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imezindua programu maalumu kwa ajili ya wanawake inayojulikana kama 'NMB Mwanamke Jasiri' yenye lengo la kuwaelimisha juu ya fursa mbalimbali zinazopatikana ndani ya benki hiyo.

Programu hiyo ilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam katika hafla iliyoambatana na kongamano maalumu la wanawake wajasiriamali iliyolenga kuwakutanisha kubadilishana mawazo juu ya fursa mbalimbali za kibiashara.

Ofisa Mkuu wa Huduma Jumuishi wa NMB, Nenyuata Mejooli, alisema programu hiyo mpya pia inawawezesha wanawake kutambua fursa mbalimbali zilizopo ndani ya benki hiyo ambazo ni mahsusi kwa ajili ya maendeleo yao, familia na taifa kwa ujumla.

Alisema benki hiyo imeamua kuja na mkakati huo kutokana na kutambua umuhimu na nguvu ya wanawake katika maendeleo na shughuli za uzalishaji.

Mejooli alisema benki hiyo inaamini kuwa wanawake wakiwa kitu kimoja na wakajua fursa zinazopatikana ndani ya NMB kama vile mikopo na elimu ya biashara watafanya mambo makubwa katika maendeleo yao kiuchumi.

"Tunatambua kwamba wanawake wengi nchini hawatumii huduma za kibenki licha ya kushiriki kwa kiasi kikubwa katika shughuli za uzalishaji na kwa kutambua na kuthamini mchango wa wanawake katika maendeleo ya taifa letu, ndiyo maana tukaamua kuja na mpango huu," alisema Mejooli.

"Na fursa ambazo zipo katika kifurushi hicho cha Jasiri kwa ajili ya wanawake ni Fanikiwa Akaunti ambayo sifa yake kubwa ni unafuu wa gharama zake ukilinganisha nyingine, NMB Mkononi, Mikopo ya Wanawake Waajiriwa (SWL), NMB Bancassurance kwa ajili ya huduma mbalimbali za bima pamoja na Dunduliza ambayo inawawezesha wanawake kujiwekea akiba kidogo kidogo kwa ajili ya bima ya afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)."

Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, Joaquine De-Mello, alisema fursa hiyo mpya itasaidia kuwakomboa wanawake nchini kiuchumi.

Alisema pamoja na wanawake kuwa wengi kitakwimu na wazalishaji wakubwa, bado ushiriki wao katika huduma rasmi za kifedha ni mdogo na usiokuwa na tija kubwa kimaendeleo.

"Sina utafiti binafsi, lakini najua kuna changamoto mbalimbali zinachangia mkwamo kwa wanaweke wengi ikijumuishwa na uelewa mdogo wa mbinu na stadi za biashara, ujasiri na kujiamini," alisema Jaji De Mello.

"Niwapongeze NMB kwa kulibeba hili na kuandaa programu maalumu ya uwezeshaji, uhamasishaji na elimu, ili nasi (wanawake) tufaidike katika huduma za kibenki hususani kukopa."

## Konstabo si Ofisa Uhamiaji

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imemfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Konstabo wa Uhamiaji kituo cha Dodoma, Elibariki Mnghani (29), kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 500,000. Cheo cha Mnghani ni Konstabo na si Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo serikali kuingilia kati ulanguzi wa saruji

JUZI Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kulishughulikia tatizo la kupanda bei kwa saruji na kukosekana sehemu mbalimbali nchini.

Aidha, alitoa siku nne (hadi Novemba 20) kwa wakuu wa mikoa kukagua viwanda na mawakala na kuwasilisha taarifa za sababu za kupanda kwa bei kwa kati ya Sh. 3,000 na 4,000.

Alisema bei hiyo imepaa wakati wa kampeni kwa kuwa baadhi ya watu (hakuwataja) walijisahau, hivyo kusababisha kupanda kwa bei.

Tunaipongeza serikali kwa kuona jambo hili ambalo liliibuliwa na gazeti hili Novemba 9, mwaka huu, kwa kufuatilia bei ya bidhaa hiyo kila mkoa na wilaya.

Baada ya kuchapishwa kwa habari hiyo, wakuu wa mikoa walifanya ziara kwenye maduka na viwanda, huku wakitoa maelekezo kwa wenye viwanda, wauzaji wa jumla na rejareja kuhakikisha bidhaa hiyo inarudi katika bei ya zamani.

Mathalani, kwa Dar es Salaam iliagizwa isiuzwe zaidi ya Sh. 15,000, lakini hadi sasa hakuna matunda ya kuridhisha kwa kuwa bado inauzwa kati ya Sh. 15,500 hadi 17,000, na sababu kubwa haijajulikana.

Mmoja wa wauzaji, alidai tatizo ni upatikanaji wa bidhaa hiyo, kwa kuwa wanalazimika kusubiri kwa mwezi mmoja tangu kuagiza kwa kuwa kwenye viwanda kuna idadi kubwa ya wanaohitaji.

Baadhi ya maduka hayana saruji na wanadai zimepita wiki tatu tangu wamaagiza na jibu linalotolewa ni bado gari yao haijafikiwa katika wanaopaswa kupata mgao husika.

Kwa sasa zinasikika kauli za viongozi wa wilaya kila mmoja akijaribu kuwabana mawakala ambao huuza jumla na wauzaji wa rejareja, lakini bado ipo haja ya kufuatilia mzizi wa tatizo hili ili kumaliza kabisa.

Kuadimika na kupanda kwa bidhaa hii kunafanana na sakata la sukari ambalo nalo lilisumbua kiasi cha baadhi ya watu kukamatwa kwa kosa la kulangua, lakini bado haikushuka na kufika katika bei ekelezi ya Sh. 2,500 na sababu kubwa ikielezwa ni wengi kuuza nje, kuficha wakati viwanda vikifanya matengenezo msimu wa mvua.

Ni wazi kuwa ni wajibu wa serikali kumlinda mlaji dhidi ya ulanguzi wowote pasipo kuingilia soko huria, jambo ambalo linatakiwa kufanyika kwa busara kubwa na kusiwe na mwanya wa kumuumiza yeyote.

Tayari baadhi ya mamlaka za vyombo vya dola zimesema zinaanza kuwasaka wafanyabiashara wanaoficha na kupandisha bei, na ndipo tunaposema busara itumike zaidi kuliko nguvu ya kuumiza watu.

Wapo ambao wanadai tatizo lipo katika upatikanaji wa bidhaa hizo, ni vyema mifumo ya serikali ikafuatilia kwa kina kwa lengo la kujua ukweli wa madai hayo, ili kama kuna walioficha baada ya kuichukua kiwandani wajulikane.

Lakini kama viwanda vyote vinazalisha inavyotakiwa kiasi cha kuuza ziada katika nchi za Burundi na Rwanda, maana yake soko la ndani limejitosheleza, na lazima kujiuliza nini kinalifanya soko hilo lisijitosheleze.


Na kama soko la ndani bado halijajitosheleza, ni vyema kusitisha kupeleka nje na kulisha soko la ndani kwanza kuhakikisha ipo ya kutosha na ndipo ikauzwe katika masoko ya nje ya mipaka yetu.

Yote yatawezekana iwapo sekta binafsi na serikali zitashirikiana vyema, kwa kukaa pamoja kujadili kiini cha tatizo, na kama upo upungufu wa kushughulikiwa zifanyike jitihada za haraka, ili kuendelea uhusiano mzuri na ushirikiano thabiti.

Tunatarajia nia ya serikali kuhakikisha bidhaa hiyo inashuka bei itatimia, na ulanguzi hautakuwapo, vinginevyo ni kuwaumiza walaji hasa wadogo ambao kwa sasa wamesitisha kujenga na kufyatua matofali ya kuuza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mnaotamani uwaziri mnaiweza kasi ya JPM?

TANGU aapishwe Novemba 5, mwaka huu kuongoza nchi kwa miaka mingine mitano, Rais John Magufuli ameteua mawaziri watatu watakaokuwa miongoni mwa wale wanaokwenda kuunda Baraza la Mawaziri.

Ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Prof Palamagamba Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Dk. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, ambao walikula kiapo Jumatatu wiki hii.

Wote watatu wamerudi kwenye nafasi walizokuwa wakizishikilia kwenye ngwe ya kwanza ya miaka mitano ya uongozi wa Rais Magufuli ambayo ilihitimishwa Novemba 28.

Wakati huu wizara nyingi shughuli zikifanywa na makatibu wakuu na wasaidizi wao, macho na masikio ya Watanzania ni kutaka kuona baraza hilo la mawaziri, wapi wamo na watakaoachwa.

Lakini tayari, mkuu wa nchi ameshaweka wazi kuwa mchakato wa kuunda baraza lake la mawaziri unakwenda polepole kuliko ilivyotarajiwa na wengi, kwa kuwa CCM ina wabunge zaidi ya 350, kama alivyodokeza.

Vilevile, Rais anasema, kuna wabunge 10 ambao atawateua hivyo, hataki haraka haraka kama mwaka 2015, kwa kuwa ilikuwa rahisi kutokana na idadi ya wabunge wa CCM kuwa ndogo.

Rais anasema, wapo wengi walioumudu nafasi zao, lakini anaona ajiridhishe kwanza, hivyo ni wazi amedhamiria kuhakikisha kila jambo linakwenda sawa katika uundwaji wa baraza hilo.

Pamoja na hayo, wakati anazindua bunge la 12 hivi karibuni, anasema mtindo wa utumbuaji majipu alioanza nao katika ngwe ya kwanza, utaendelea kama kawaida kwa watumishi ambao hawatatimiza wajibu wao.

Katika muhula wa kwanza ikulu Rais alikuwa akilifanyia mabadaliko ya mara kwa mara ya baraza lake kwa kuwaondoa mawaziri ambao walishindwa kwenda na kasi yake.

Wengine waliondolewa na kurejeshwa wapo pia waliotumbuliwa moja kwa moja na waliokwenda na kasi yake wamedumu kwa miaka mitano ya ngwe ya kwanza.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, katika suala la maendeleo, Rais hakusita kubadili baraza la mawaziri mara kwa mara kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuwaweka pembeni baadhi yao walioshindwa kufuata kasi yake.

Kwa sasa ni kama mawaziri wamepumua baada ya kazi kubwa ya miaka mitano ya kwanza, ingawa inawezekana baadhi yao wako kwenye wasiwasi kuwa huenda wasiwamo katika baraza jipya.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, wapo baadhi ya mawaziri waliodumu kwa miaka mitano ya awamu ya kwanza, lakini hiyo isiwe tiketi ya kuwapa uhakika wa kuendelea na safari.

Lakini pia wengine walitoswa na kisha wakarejeshwa, kuhamishwa wizara na wengine kutumbuliwa na wote hao wakati huu inawezekana kila mmoja roho iko juu kwa kutojua baraza jipya litakuwa na sura gani.

Kwa hali kama hiyo, ni wazi vichwa vitakuwa vinawauma kwa kuwaza kama watarudi ama Rais ataongeza sura nyingi mpya na kuacha za zamani anapoanza ngwe ya pili.

Lakini pia, ni vyema wanaotaka uwaziri watambue kuwa mwenye macho haambiwi tazama kwa kuwa kasi ya utendaji ya JPM iko wazi, hivyo wale wanaotamani kuwa mawaziri, hawana budi kujihoji kwanza.

Je, wanaweza kwenda na kasi ya JPM? Kwa kuwa ameshajipambanua kuwa ni mtu wa kuchapa kazi tu, hivyo Muungwana anapolonga, anatarajia kuwa wale watakaoteuliwa watamsaidia kufanya kazi kulingana na matakwa yake.

Kwa kuangalia utendaji wake uliopita, wanaotaka uwaziri watajua ni nini ambacho anakitaka kutoka kwao, ili kuharakisha maendeleo ya watu na taifa.

Katika suala la kuleta maendeleo, Rais Magufuli hasiti kuwatumbua wale wanaoonekana kwenda kinyume na kasi yake, hivyo wasije kushangaa watakapojikuta wakiwekwa pembeni, kuhamishwa wizara ama kumalizia muhula wa pili.

Hivyo, kwa kuangalia utendaji wake uliopita, wanaotaka uwaziri watajua ni nini ambacho Rais anakitaka kutoka kwa wateule wake, kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya taifa.

# Shule zaonywa vishoka wa umeme

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapa limeonya uongozi na wamiliki wa shule, kuacha kutumia mafundi wasio na taaluma kufunga umeme kwenye shule zao.

Limesema baadhi ya shule zinatumia mafundi wasio na taaluma kufunga umeme kwa ajili ya kukwepa gharama, na kusababisha kuendelea kuwapo na majanga ya moto kwenye shule.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Shinyanga, George Mrutu, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa wamefanya ukaguzi na kutoa elimu ya majanga ya moto kwa shule 30.

Alisema ni vyema uongozi na wamiliki wa shule wawe wanatumia mafundi wenye taaluma kufunga umeme kwenye majengo badala ya kutumia mafundi wasio na uwezo na hatimaye kusababisha kuendelea kwa majanga ya moto.

"Baada ya kufanya ukaguzi kwa shule 30 na kutoa elimu ya majanga ya moto, napenda kutoa ushauri kwa uongozi wa shule, kuwatumia mafundi umeme wenye taaluma, ili kuzuia majanga ya moto yatokanayo na uzembe," alisema Mrutu.

"Mapendekezo mengine ni uongozi wa shule kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mabweni ili kubaini wanafunzi wanaomiliki vifaa vya umeme, pia kuweka ulinzi wa kutosha na kuzuia hujuma za kuchoma shule," alisema.

Katika hatua nyingine ametoa wito kwa viongozi na wamiliki wa shule, kukaa na kumaliza migogoro baina yao na wafanyakazi, pamoja na jamii inayozunguka shule, ili kumaliza tofauti zao, zinazoweza kusababisha kuzuka kwa majanga hayo.




Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Joaquine De-Mello (wa pili kushoto), Ofisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori (katikati), pamoja na Ofisa Mkuu wa Huduma Jumuishi, Nenyuata Mejooli, wakionyesha vipeperushi wakati wa uzinduzi wa 'NMB Mwanamke Jasiri', jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana sasa wahimizwa kuchangamkia fursa kilimo

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, amewataka vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea, kujitokeza na kujiandikisha kwenye ofisa za serikali za vijiji, mitaa na kata ili kupata ruzuku za kilimo bure.

Ruzuku za pembejeo zinazotolewa bure ni pamoja na mbolea za kupandia (NPK), mbegu za mahindi, alizeti na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia pamba na wanaotakiwa kupata ruzuku hizo ni vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35.

Msumba aliyabainisha haya jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake huku akibainisha kuwa kila mwaka wa fedha, halmashauri imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kununua ruzuku za kilimo na kuzigawa bure kwa vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano za mazao ya chakula na biashara. Alisema mwaka huu wa fedha 2020/21, halmashauri imetenga Sh. milioni 72 kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano.

Kutokana na hali hiyo, alisema vijana wanatakiwa wakajiandikishe na kukaguliwa mashamba yao na maofisa kilimo ili kupata ruzuku hizo bure.

"Halmashauri zote nchini, pekee inayotoa ruzuku za kilimo bure kwa vijana ni halmashauri yetu. Mvua zimeanza kunyesha na vijana wanatakiwa kuchangamkia fursa hii ya bembejeo bure kwa ajili ya kilimo chenye tija hasa kwenye mazao ya chakula na biashara," alisema Msumba.

Pia alisema wakati wa ukaguzi wa maeneo, maofisa kilimo ni wakushauri ni mazao ya aina gani wanatakiwa kulima na watakuwa wanawatembelea mara kwa mara kwa ajili kuwapatia ushauri wa kitaalamu na mazao watakayopata si mali ya halmashauri bali ni yako mwenyewe.

Katika msimu uliopita, Msumba alisema halmashauri ilitenga Sh. milioni 50 za kununua pembejeo, lakini walijitokeza vijana wachache kulinganisha na idadi ya vijana walioko wilayani hapa, hatua iliyosababisha kutumika Sh. milioni 17 pekee.

Pia alisema sababu ya vijana wengi kushindwa kujitokeza kwa wingi kuchukua pembejeo zinazotolewa kila mwaka ni wengi kuhitaji fedha taslimu jambo ambalo badala ya kuzielekeza kununua pembejeo watazielekeza kwenye matumizi ya starehe.

# CAMFED yatoa elimu afya uzazi

**Na Dotto Mwaibale, SINGIDA**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la CAMFED limewataka wasichana mkoani hapa kutobweteka na badala yake kutazama fursa zinazowazunguka na kuzigeuza kuwa chanzo cha kuinua kipato katika muktadha chanya wa kuibadili jamii kimaendeleo.

Imeelezwa mkakati mmojawapo utakaowasaidia wasichana hususani wale waliojifungua katika umri mdogo ni kuwawezesha kwa kuwajengea misingi ya kutambua haki ya kupata elimu juu ya afya ya uzazi na Ukimwi.

Akizungumza mkoani hapa juzi wakati wa mafunzo ya kuwawezesha kujitambua na kutambua fursa mbalimbali zinazowazunguka nje ya mfumo rasmi wa elimu, Mkuu wa Miradi kutoka CAMFED, Nasikiwa Mwalisu, alisema mtoto wa kike akijilinda na kuwa na utambuzi wa magonjwa, atakuwa na nafasi kubwa ya kufanikiwa na kutimiza ndoto zake za maisha.

"Kundi hili kama lisipoangaliwa kwa makini na kupewa elimu hii ya utambuzi juu ya mambo mbalimbali, ikiwamo elimu ya uzazi na kujikinga na magonjwa, linaweza kupoteza mwelekeo ambao madhara yake huwa ni makubwa. Lakini pia athari zake husambaa kwa jamii na taifa kwa ujumla," alisema Mwalisu.

Kuhusu sera ya ulinzi na usalama wa mtoto, Mwalisu alisema jamii inapaswa kutambua na kuheshimu takwa hilo la msingi la mtoto kupata elimu, kuheshimiwa, kupendwa na kulindwa kama haki ya msingi na sio hiari, lengo hasa ni kujenga ustawi na taswira chanya ya ukuaji wake kisaikolojia na kiafya.

Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, Yasinta Alute, alisema afya njema ni matokeo ya kila kitu katika maisha na ustawi wa ukuaji wa mtoto.

Alisisitiza kuwa kama rika hilo la mtoto wa kile litapatiwa mafunzo ya mara kwa mara juu ya utambuzi kwenye nyanja mbalimbali, ni dhahiri litageuka chachu katika kuleta maendeleo kwenye jamii.

"Ukipata mafunzo ya afya ya uzazi na ukajitambua huwezi kukosea wala kurudia tena makosa. Nawaomba ninyi mliobahatika kupata mafunzo hayo mkawe chachu na mabalozi kwa wengine," alisema Alute.

Muuguzi huyo mkuu pia aliwaomba CAMFED kuangalia namna ya kupanua wigo wa huduma zao kwenye wilaya zingine mkoani hapa ili vijana wengi zaidi kunufaika.

Awali, Ofisa Elimu Sekondari na Mwenyekiti wa Kamati ya Wilaya ya CAMFED Manispaa ya Singida, Omary Kisuda, alisema wasichana 60 kutoka Singida Manispaa na Wilaya ya Manyoni wanaendelea kupewa mafunzo kupitia programu ya elimu ya utambuzi kwa mtoto wa kike yaani 'Tanzania Campaign for Female Education'

"Hili ni rika la wao kujiendeleza kielimu, biashara, ujasiriamali na elimu ya afya ya uzazi na ndiyo sababu hasa ya kuwakutanisha na kuwapa mafunzo haya muhimu ya utambuzi chini ya ufadhili wa CAMFED na serikali," alisema Kisuda.

# Azania, DSE kuhamasisha wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Azania kwa kushirikiana na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) wamezindua shindano ambalo litawaongezea vijana uelewa wa masuala ya uwekezaji katika kampuni zilizosajiliwa katika soko hili nchini.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo uliofanyika Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Azania Bank, Charles Itembe na Mwanasheria Mkuu wa DSE, Mary Mniwasa, walisema shindano hilo liitwalo DSE Scholar Investment Challenge ni chachu ya kuwahamasisha siyo wanafunzi tu bali vijana kushirika katika uwekezaji kwenye soko la hisa.

Itembe alisema Benki ya Azania ambao ni wadhamini wakuu wa shindano hilo inalitazama shindano hilo kama moja ya fursa kwa vijana hasa wanafunzi wa elimu ya juu kuweza kuongeza uelewa katika masuala ya fedha, masoko ya fedha na namna masoko hayo yanavyofanyakazi kwa kuwa mchakato huu unahusisha kutoa elimu kuhusu masuala hayo.

"Benki ya Azania inaona hii kuwa ni fursa ya kushiriki katika kuunganisha baina ya vijana na soko la ajira nchini, huku mantiki kubwa ikiwa ni kuinua kiwango cha elimu kwa vijana wa Kitanzania na kuwajengea utayari wa kuajiriwa wakiwa na weledi wa kutosha," Itembe alisema. Mkurugenzi huyo wa Azania Bank aliongeza kwamba udhamini huo ni moja ya mambo makuu yaliyomo katika sera benki ya kusaidia jamii (CSR policy). "Sera yetu ya kusaidia jamii imejielekeza katika mambo makuu manne ambayo ni kusaidia jamii katika mambo ya elimu na uelewa kuhusu mambo ya fedha, kusaidia vijana na mambo yanayowaendeleza vijana kwa ujumla," alisisitiza Itembe.

Naye Mwanasheria Mkuu wa DSE, Mniwasa, alisema taasisi yao imekuwa ikiendesha mashindano hayo tangu mwaka 2014 kwa lengo la kuelimisha jamii. Akifafanua kuhusu ushiriki, Mniwasa alisema, "kwanza utapaswa kupakua App inayoitwa DSE-SIC (inayopatikana kwenye simu zote za mfumo wa Android) na kujisajili kwa kuweka taarifa zako muhimu ikiwamo majina yako, namba zako za simu, barua pepe yako nk." Kila mshiriki atapewa mfano wa fedha 3m/-kama mtaji wa kuanzia na kuonyesha ni jinsi gani ataweza kuziwekeza na kuzizalisha kwa njia mbalimbali kama vile kushiriki katika manunuzi na mauzo ya hisa kwa vitendo.

"Hatimaye mshiriki ambaye ataweza kuzalisha zaidi ndiye atakayekuwa mshindi," alisisitiza Mniwasa na kuongeza kwamba shindano linatarajia kufikia tamati mwisho wa mwezi Desemba mwaka huu.



Wanafunzi wakigombea kuingia kwenye daladala katika kituo cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, mara kwa mara huachwa na makondakta vituoni na kusababisha usumbufu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wataka kampeni chakula shuleni kukuza ufaulu, kupunguza udumavu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

BAADHI ya wakazi wa Mailimoja katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wameomba ifanyike kampeni ya kuchangia chakula shuleni, ili kuondoa udumavu kwa watoto na kukuza ufaulu.

Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti na Nipashe, wananchi hao walisema maagizo yanayotolewa na baadhi ya viongozi hayawezi kutekelezwa kwa wakati endapo hakutakuwa na kampeni ya kuhamasisha itakayoanzia kwenye mitaa.

Phillemon Mabuga, mkazi wa Tangini, mjini hapa, alisema suala la watoto kupata chakula shuleni ni la kupewa kipaumbele kuanzia kwa wenyeviti wa mitaa ambao watatakiwa kuitisha mikutano na kuiweka kama ajenda yao.

Mabuga alisema kila jambo ambalo uhamasishaji wake unaanzia kwenye ngazi za chini, linakuwa na matokeo chanya, hivyo suala la watoto kupata chakula shuleni katika mapambano ya kuondoa udumavu na kuinua kiwango cha ufaulu ni la muhimu na hakuna mwananchi atakayepinga.

Naye Ester Charles, mkazi wa Muheza Kata ya Mailimoja, alisema suala la chakula shuleni ni la kuungwa mkono na kwamba pale ajenda hiyo itakapofikia, wananchi wataipitisha kwa manufaa ya watoto wao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tangini, Primin Gama, alisema ajenda ya chakula shuleni hawakuwahi kuizungumzia kwenye mikutano na wananchi, lakini kwa sasa wataiweka ili watoto hususani wa darasa la tatu hadi la saba watapata chakula.

Gama alisema chakula shuleni ni jambo la muhimu kwa kuwa mbali na kuepuka udumavu, pia litasaidia kuondoa utoro kwa sababu wapo baadhi ya wanafunzi wanakwenda shuleni bila kupata chai, hivyo kushindwa kumudu kukaa darasani kwenye vipindi vyote vya masomo.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Pwani, Pamela Meena, alisema kwa sasa hali ya udumavu kwa mkoa imefikia asilimia 23.8 huku takwimu za kitaifa zikiwa ni asilimia 31.8.

Pamela alisema kwa sasa elimu inaendelea kutolewa kwenye vituo vya afya vinavyotoa huduma ya mama na mtoto, ili kutokomeza udumavu na utapiamlo kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

Hata hivyo, alisema pia wanasisitiza watoto walioko shuleni kupata chakula kwa kuwa hali ya kushinda na njaa mara nyingi inasababisha wawe kwenye hatari ya kupata udumavu wa akili na mwili.

# Nchi tano kushiriki kongamano la mbegu

**Na Faustine Feliciane**

NCHI tano kutoka Afrika na Ulaya, zinatarajiwa kushiriki kongamano la kimataifa la kilimo hai lililopangwa kufanyika Novemba 23, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Kongamo hilo litakalojadili 'Uhuru wa Mbegu na Utunzaji wa Bioanuai', limeandaliwa kwa pamoja Taasisi ya Mwavuli wa Kilimo Hai Tanzania (TOAM) na Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali na sekta binafsi inayojishughulisha na Utunzaji Bioanuai ya Kilimo Tanzania (TABIO).

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TOAM, Bakari Mongo, alisema kongamano hilo litawaleta pamoja washiriki mbalimbali kutoka serikalini na vyuo vikuu.

"Mazao yaliyobadilishwa vinasaba yamekuwa yakipigiwa chapuo kama suluhisho la changamoto katika kilimo hapa Tanzania. Wakati ikielezwa kuna faida kwenye mbegu hizo pia kuna athari za kijamii na kiuchumi zinazoambatana na matumizi yake ambazo idadi kubwa ya watu hawazifahamu," alisema Mongo.

Alisema kongamano hilo litajadili athari hizo na umuhimu wa usalama wa mbegu kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Mratibu wa TABIO, Abdallah Mkindi, alisema mbegu ni kiunganishi cha kwanza katika mnyororo wa chakula, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuzilinda na kuzirithisha kwa vizazi vijavyo.

Alisema serikali kwa upande wake itakuwapo kwenye kongamano hilo kusikia majadiliano kutoka kwa wakulima juu ya usalama wa mbegu.

Kongamano hilo la siku moja litafanyika kwenye ukumbi mpya wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

# Watakiwa kuzingatia sheria za mazingira

Na Yasmine Protace, MKURANGA

WAKAZI wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wametakiwa kuzingatia maelekezo ya serikali yanayolenga kuepukana na majanga ya moto, sambamba na mafuriko.

Akizungumza na wanafunzi wa Kundomlanzi Kata ya Bupu 'B', Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Mkuranga, Francisico Chungi, aliwataka wakazi wote wa vijiji 165, kuepuka kupalilia mashamba yao kwa kuyachoma moto.

"Kitendo cha kushindwa kupalilia mashamba na kuchoma moto, kimechangia kuunguza mashamba ya jirani ikiwamo na kuungua kwa nyumba," alisema kamanda huyo.

Chungi pia aliwataka wananchi hao kuacha utamaduni wa kuchoma mkaa jirani na barabara.

Pia aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kufunika visima vya maji, na kueleza kuwa hatua hiyo inssaidia kuepusha maafa ambayo yanaweza kutokea kwa jamii.

Kadhalika, aliwataka walimu wa shule za serikali na binafsi, kuwa na vifaa vya kuzimia moto, ikiwamo na kuondoa paa chakavu katika hosteli.

Mkazi wa Kidemvule Mkuranga, Abdull Khareem, aliiomba Wizara ya Mambo ya Ndani kuwasaidia gari la Zimamoto, ikiwamo na vitendea kazi katika ofisi ya zimamoto wilayani humo.

Aliongeza kuwa Mkuranga ambayo ina viwanda vikubwa na vidogo zaidi ya 80, inategemea gari la Zimamoto kutoka Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam.

**Kitendo cha kushindwa kupalilia mashamba na kuchoma moto, kimechangia kuunguza mashamba ya jirani ikiwamo na kuungua kwa nyumba.**

# Polisi yaagizwa kukagua kampuni binafsi za ulinzi

Na Frank Kaundula, MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imelitaka Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi katika kampuni zote za ulinzi mkoani kudhibiti udanganyifu unaofanywa na baadhi ya kampuni hizo hasa kuajiri walinzi ambao hawajapitia mafunzo yoyote ikiwamo matumizi ya silaha.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, katika ufunguzi wa mafunzo ya programu unganishi ya walinzi binafsi nchini yanayotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Tanzania Private Security Integration Service TPSIS kwa kampuni za ulinzi na walinzi binafsi

Alisema pamoja na miongozo mbalimbali ya kisheria iliyoelekezwa, bado kumekuwa na ukiukwaji wa sheria kwa baadhi ya kampuni za ulinzi hasa kwa kuajiri watu wasio na weledi, huku wengine wakitumia fursa hiyo kujihusisha na vitendo vya kihalifu.

**Pamoja na vikwazo mbalimbali vinavyotajwa, upo mchango wa kampuni za ulinzi binafsi katika kuimarisha usalama kupitia dhana ya ulinzi shirikishi.**

"Ni lazima Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi wa kina kwenye kampuni zote, ili kuhakiki kama wanakidhi vigezo vya kutoa huduma za ulinzi na kama hawakidhi, basi wafungiwe mara moja, kwa sababu kuna shaka baadhi ya kampuni zinafanya kinyume cha matakwa ya kisheri kwa sababu hawana mafunzo," alisema Msulwa.

David Rwegasore, mtendaji mkuu wa programu unganishi ya walinzi binafsi (TPSIS), alisema mafunzo hayo ya siku nne ambayo yanahusisha washiriki 49 kutoka kampuni mbalimbali za ulinzi za ndani na nje ya Mkoa wa Morogoro.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo yalilenga kuongeza ufanisi katika kutekeleza azima ya kuimarisha usalama katika jamii na kuwafanya watu wa kada ya ulinzi kuaminika katika utendaji wake wa kazi baada ya kuhitimu mafunzo ambayo yanashirikisha Jeshi la Polisi.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi kutoka makao makuu, Narcis Missama, alisema pamoja na vikwazo mbalimbali vinavyotajwa, upo mchango wa kampuni za ulinzi binafsi katika kuimarisha usalama kupitia dhana ya ulinzi shirikishi.




Mchuuzi wa madafu akisaka wateja kwenye mvua kubwa katika eneo la Posta, jijini Dar es Salaam jana. Dafu moja aliliuza kwa bei ya 1,000/-. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yaombwa madarasa ya Memkwa

Na Christina Haule, MOROGORO

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeombwa kuona umuhimu kuweka madarasa mawili kwenye kila shule ya msingi nchini kwa ajili ya wanafunzi wa Memkwa.

Madarasa hayo imeelezwa kuwa yatawasaidia watoto wa mitaani kwa kiasi kikubwa, ili kuboresha suala la elimu kwa watu wote nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwere 'A', iliyopo Manispaa ya Morogoro, Nivocavity Monyo, alisema licha ya kuwapo kwa uchache wa vituo vya kufundisha watoto wa mitaani, lakini vilivyopo vingi vinamilikiwa na watu binafsi ambao wakati mwingine wanashindwa kuviendeleza na kuacha jukumu hilo likishikwa na shule za msingi baada ya kupitia utaratibu kisheria.

Alisema moja ya darasa la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu linalomilikiwa na kituo cha Faraja Trust Fund kimelazimika kusimamiwa na Shule ya Msingi Mwere 'A' kwa miaka 2 mfululizo sasa baada ya mmiliki wa kituo hicho kushindwa kukiendesha kutokana na sababu mbalimbali.

Mwalimu Monyo alisema kwa sababu ya uwapo wa watoto wa mitaani wenye mahitaji ya elimu na misaada mbalimbali kupitia serikali za mitaa, madarasa hayo yatasaidia watoto hao kupata elimu ambayo wengi huwa wanaikosa mapema na kuingia kwenye vituo wakiwa na miaka 9-14, jambo ambalo huwapa ugumu wa kuwasaidia hasa wale walioingia na miaka 14 kufuatia kuwa katika hatari ya kutofanya mtihani wa darasa la nne ili waendelee na masoko.

Naye mwalimu wa kituo cha Memkwa, Nora Makuga, alisema kituo hicho kilianzishwa kwa ajili ya watoto waliokuwa kwenye mazingira magumu wakiwamo wa mitaani ambapo kufuatia changamoto za chakula, mavazi na vifaa vya kujifunzia na kufundishia shuleni hapo watoto 6 wa mitaani wameacha kuendelea na masomo kwa mwaka 2019 kila mwaka kufika kituoni kwa ajili ya kupata elimu.

Makuga alisema, mwaka 2020 kituo hicho kimepokea wanafunzi 21 walitoka kwenye mazingira magumu ambao ni wasichana 4 na wavulana 17 ambao mpaka sasa wanaendelea na masomo.

Naye Mkurugenzi wa Faraja Trust Fund, Dk. Lucy Nkya, alisema Faraja ilianza kuwasaidia watoto hao wanaoishi katika mazingira magumu tangu mwaka 1998 wakianzia na watoto 250 waliowafundisha chini ya mti nje ya jengo la Faraja kufuatia wingi wa watoto wa mitaani.

Dk. Nkya alisema baada ya kuona mwitikio wa kutaka kusoma waliomba ofisi ya elimu manispaa na kuweza kupata walimu wawili ambao walianza kutoa elimu hiyo katika jengo lake lililopo jirani na Shule ya Msingi Mwere 'A'.

Alisema dhana ya kuwakusanya watoto hao kuwapa elimu ilileta maana kwa sababu wengi wa watoto hao walibadilika kuacha tabia za kikatili, ubakaji, ulawiti na uvutaji sigara na kuwa watoto watiifu.

# RC awapa jukumu walimu vijana kuwa wazalendo

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

WALIMU mkoani Tabora, wametakiwa kushirikiana na jamii, ili kuwajenga vijana katika misingi ya uzalendo.

Wametakiwa wawajenge katika uzalendo utakaowafanya kuipenda nchi yao na kuwa tayari kuleta maendeleo kwa kutumia akili na vipaji vyao.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati wa uzinduzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Arba Light iliyopo Manispaa ya Tabora.

"Jitahidini kuwaandaa wanafunzi kuwa wazalendo ambao watakuwa na uchungu kwa nchi yao na hawako tayari kuwa vibaraka wa watu mengine," alisema.

**Wanafunzi watakiwa kujengwa katika nidhamu na weledi ambao utawafanya kuwa tayari kufanya kazi kwa moyo wao wote kwa ajili ya kuipeleka nchi mbele.**

Aliongeza kuwa wanafunzi watakiwa kujengwa katika nidhamu na weledi ambao utawafanya kuwa tayari kufanya kazi kwa moyo wao wote kwa ajili ya kuipeleka nchi mbele.

"Hatutarajii miongoni mwa wanafunzi mnaowafundishi tupate vibaraka wanaotumika kuiharibu nchi yetu na mkoa wetu...hatutarajii tupate vijana kutokana na hao watakaokuwa chanzo cha mitafaruku nchini," alisema.

Dk. Sengati alisema vijana wanatakiwa kulelewa toka awali katika misingi ya uzalendo halisi wa Kitanzania ambao wako tayari kutetea misingi ya kijamaa iliyojengwa toka uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere hadi uongozi wa sasa wa Dk. John Magufuli kwa kuwatetea wanyonge.

"Tuendelee kuwalea vijana katika misingi mizuri...hakuna rasilimali muhimu kama binadamu, ukikosea katika malezi ya vijana toka awali, pia katika elimu utatengeneza kijana asiyekuwa na misingi ya utaifa...kijana asiyekuwa na misingi ya uzalendo na asiyeelewa kuwa hana nchi nyingine zaidi ya Tanzania na tutakuwa tumepoteza mwelekeo wao," alisema.

Dk. Sengati alisema ni lazima walimu na jamii waendelee kutengeneza vijana ambao watatumia akili na vipaji vyao katika kuhakikisha wanaliendeleza na kulitetea Taifa lao.

# Wahitimu afya CUHAS wafundwa

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WAHITIMU 620 katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya (CUHAS) Bugando jijini Mwanza, wameaswa kuzitumia vema taaluma zao katika kutoa huduma kwa wananchi bila kinyongo wala ubaguzi.

Akiwatunuku wahitimu hao vyeti vya taaluma mbalimbali, Askofu wa Jimbo la Geita, Mhashamu Flavian Kassala, aliyemwakilisha Mkuu wa Chuo, alitoa ushauri huo juzi katika mahafali ya 13 yaliyofanyika katika viwanja vya Bugando jijini hapa.

"Nawaombeni mwendako mkazitumie vema taaluma zenu kutoa huduma kwa wananchi bila kinyongo au ubaguzi, mkawe mfano wa kuigwa kwa jamii kuwa na maadili mema," alisema Askofu Kassala.

Wahitimu wengine 214 kati ya hao walitunukiwa stashahada za taaluma mbalimbali, huku 30 wakihitimu shahada za uzamili pamoja na mmoja shahada ya uzamivu (PhD), ambaye ni daktari bingwa mwanamke na mhadhiri chuoni hapo.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Paschalis Rugarabamu, alisema wahitimu wengine 375 walitunukiwa shahada ya kwanza.

Aidha, Rugarabamu aliisifia familia ya mume na mke ambao ni madaktari waliohitimu PhD wote mwaka mmoja na kuwa mfano wa kuigwa na kujifunza watu wengine katika chuo hicho kwa uthubutu wa kujiendeleza kielimu zaidi.

**Nawaombeni mwendako mkazitumie vema taaluma zenu kutoa huduma kwa wananchi bila kinyongo au ubaguzi, mkawe mfano wa kuigwa kwa jamii kuwa na maadili mema.**



Mkazi wa jijiini Dar es Salaam akivuka barabara iliyojaa maji ya mvua, ambayo mitaro yake imezibwa na uchafu na kusababisha maji kutopita kwa urahisi. **PICHA: MAKTABA**

# Dawa ya mafuriko Dar yabainishwa

**Na Mwandishi Wetu**

IMEELEZWA kuwa changamoto ya mafuriko ambayo imekuwa ikilikabili Jiji la Dar es Salaam inaweza kupata ufumbuzi ikiwa itatumika teknolojia ya kisasa, yakiwamo mabomba yenye viwango.

Ushauri huo ulitolewa na Alimiya Osman, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa kampuni ya utengenezaji wa mabomba ya Plasco Limited, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusiana na hali ya mafuriko jijini.

Alisema Jiji la Dar es Salaam limekuwa hatarishi kutokana na changamoto ya mafuriko ambayo imekuwa ikiwasababishia wakazi wake usumbufu mkubwa, hata ikinyesha mvua kwa muda mfupi maeneo yake mengi yamekuwa yakijaa maji na barabara nyingi kupitika kwa shida kutokana na kujaa madimbwi ya maji.

Alisema mara nyingi mafuriko katika maeneo ya mijini katika nchi mbalimbali duniani, yamekuwa yakisababishwa na mifumo mibovu ya miundombinu ya mifereji ya maji, kutofanyiwa ukarabati mifumo hiyo, utumiaji wa mabomba yenye viwango duni na uwekezaji katika miundombinu ya kusafirisha taka na mvua kuwa mdogo ama kutofanyika kabisa.

Alisema mabomba wanayoyatengeneza aina ya weholite yanaweza kuwa suluhisho ya mafuriko kwa kuwa ni imara, mepesi, yana kipenyo kikubwa, yametengenezwa na malighafi zenye ubora.

Pia Osman alisema yanafaa kutumika wakati maji yanakuwa na msukumo mdogo kwenye ujenzi wa miundombinu ya mifumo ya majitaka, mifumo ya utakatishaji wa majitaka, kutengeneza makaravati, mabomba ya kupeleka na kupitisha maji baharini na usambazaji wa maji katika miradi ya umwagiliaji.

"Matumizi yote haya yanafanya mabomba haya kufaa kutumika sio kwenye miradi ya manispaa bali pia kwa matumizi ya viwandani," aliongeza.

"Plasco ndio kampuni pekee yenye leseni ya kutengeneza mabomba yanayotumia teknolojia ya weholite nchini na ni ya ubora mkubwa kiasi cha kuhimili changamoto ya mafuriko katika maeneo ya mijini."

Alisema wamekuwa wakifanya kazi na manispaa za Tanzania na sekta binafsi kupitia kampuni za ujenzi zinazojenga miradi mbalimbali kwa kutumia mabomba hayo.

Mifumo ya weholite imetajwa ni suluhisho jipya la ubunifu wa bomba ambalo linaweza kuleta thamani kubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam, kwani yanatengenezwa nchini kwa kutumia teknolojia za viwango vya kimataifa ambazo zimekuwa zikitumika katika nchi za Afrika Kusini, Ulaya, Amerika Kaskazini na Tanzania.

Uhasama majimboni, ‘miba njiani’, corona vibano vilivyokwaza kinamama Zanzibar

Ukurasa 12





Ukurasa 13

**Ni dhana inayowahusu wote waliopigiwa na wapigakura**



KILIO RUZUKU

# Ajabu vyama bila vigezo kulilia huruma ya serikali

**Na Sabato Kasika**



John Cheyo



Augustino Mrema



Queen Sendiga

BAADHI ya vyama vya siasa kwa muda mrefu vimekuwa vikilalamikia kukosa ruzuku inayotolewa na serikali, huku vikidai kuwa ukata unavisababishia vishindwe kutekeleza majukumu ya kisiasa ipasavyo.

Malalamiko ya baadhi ya vyama hivyo yamekuwapo tangu baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, uliofanyika mwaka 1995.

Ikumbukwe kuwa, kwa dhamira ya serikali, katika mwaka huo wa uchaguzi, ilitoa ruzuku kwa vyama vyote vya siasa ambavyo vilikuwa na usajili wa kudumu, ili viwezeshwe kikamilifu kushiriki uchaguzi.Lakini baada ya uchaguzi huo, serikali iliweka utaratibu rasmi wa utoaji wa ruzuku hiyo na kusababisha baadhi ya vyama kuikosa ndiyo maana hata sasa vinaililia.

Iliondoa ruzuku kwa baadhi ya vyama na kuweka utaratibu wa kisheria wa utoaji wake kutokana na sababu mbalimbali, hasa matumizi mabaya ya fedha hizo na migogoro ndani ya vyama ya kuigombania.

Mfumo uliowekwa na serikali, ni kwamba, ili kupata ruzuku, vyama vinatakiwa kupata kura ushindi wa angalau asilimia tano ya kura zote pamoja na kuwa na wawakilishi bungeni.

Tangu uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, vyama vichache ambavyo vimekuwa vikipata matokeo mazuri kwenye uchaguzi, vilianza kupata ruzuku, vikiwamo vya CUF, ACT-Wazalendo, CCM, NCCR-Mageuzi na CHADEMA.

**MAELEZO KISHERIA**

Kifungu cha 16 cha Sheria ya Vyama vya Siasa, namba 5 ya mwaka 1992 (iliyofanyiwa marekebisho) kinaeleza vigezo vinavyotumika, ili chama kipate ruzuku ni kuangalia matokeo ya uchaguzi kuona kama kimepata asilimia tano ya kura na kushinda nafasi za ubunge ama udiwani.

Ruzuku ya vyama vya siasa ni fedha ya vyama vya siasa vinavyopewa na serikali kwa ajili ya kusaidia shughuli za uendeshaji wake.

Na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ndiyo yenye jukumu la kugawa ruzuku ya kila mwezi kwa vyama vya siasa vyenye sifa kwa mujibu wa sheria.

Chama kinachopata ruzuku kinaweza kuikosa iwapo kitapoteza kwa namna yoyote ile mbunge ama diwani anayewezesha kuzipata fedha hizo.

Aidha, kitapoteza sifa kikifutiwa usajili wa kudumu, kwa hali hiyo ni wazi kwamba, chama kisichokuwa na mbunge ama diwani, hakina sifa ya kupata ruzuku, badala yake kinatakiwa kutafuta njia nyingine halali za kukisaidia za kujiendesha.

**NDANI YA VYAMA**

Pamoja na kwamba suala la utoaji ruzuku kwa baadhi ya vyama vilivyotimiza vigezo lipo kisheria, baadhi vimekuwa vikilalamikia kuikosa na kuiomba serikali ivipatie, kwa madai ya kutaka kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Katika hafla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kumkabidhi cheti cha ushindi Rais John Magufuli jijini Dodoma hivi karibuni, vyama hivyo vinarudia kukumbushia umuhimu wa kupatiwa ruzuku.

Vinamuomba rais kuviwezesha ili kusaidia shughuli za kiutendaji, japo kwa asilimia kidogo, ili kusaidia kufanya shughuli za kiutendaji ndani ya vyama hivyo.

Aliyekuwa mgombea urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, ndiye anatoa ombi hilo, kwamba rais avifikirie vyama hivyo na kama inawezekana vipatiwe chochote ili vifikie malengo ya kuwafikiaWatanzania.

Suala la kuomba kupewa rukuzu si la mgombea huyo tu bali na viongozi wa vyama vingine ambavyo haviipati akiwamo, Mwenyekiti wa Chama cha TLP, Augustine Mrema, ambaye anaiomba serikali kuangalia umuhimu wa kuvipatia vyama vidogo vya siasa fedha hiyo ili navyo viweze kujiendesha.

Amewahi kutoa ombi hilo wakati akizungumza na wanahabari jijini Dodoma na kusema, kuna haja ya kutoa nafasi sawa kwa vyama vya siasa vidogo na vikubwa, kwa madai kwamba, vyote vinafanya siasa za kulijenga taifa.

**LAZIMA RUZUKU?**

Pengine kuna umuhimu kwa vyama vya siasa kupata ruzuku, lakini si kila chama, hivyo ni muhimu vikajitahidi kufikia vigezo vilivyowekwa na sheria badala ya kusubiri huruma ya serikali.

Vyama visivyo na uwakilishi vinatakiwa kujipanga kwa ajili ya kujenga mtandao wa wanachama, wadau pamoja na kuweka mikakati ya kusaka fedha kupitia njia mbalimbali.

Mbinu mojawapo ya kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya serikali ni michango ya wanachama, harambee na kuchangiwa na marafiki na hata kuuza kadi, kofia, sare, bendera, vipeperushi, michango ya wanachama na kuweka vitega uchumi.

Viongozi wa vyama watambue kuwa viwango vilivyowekwa na sheria vinasaidia kuvifanya kuwa makini katika ufanyaji siasa na hatimaye kufikia vigezo vinavyotakiwa kama ambavyo baadhi ya vyama vimefikia.

Si vibaya kujiuliza, kwa nini baadhi ya vyama vimefanikiwa kupata rukuzu, vina nini na vingine vimeshindwa vina tatizo gani? Viongozi hawana budi kujitafakari na kisha kuchukua hatua za kuviwezesha kupata rukuzu.

Wakumbuke kuwa fedha za umma zina majukumu mengi kuanzia huduma za jamii, ukarabati na ujenzi wa miradi na miundombinu mbalimbali inayohitaji fedha nyingi na si kuchangia vyama na wanasiasa ambao hawana wawakilishi wala hawajatimiza vigezo kisheria.

Ni vyema vyama visivyo na ruzuku vitambue kuwa fedha hizo ni kodi ya Watanzania, ambayo ina matumizi mengi ikiwamo kulipia elimu bure, mikopo kwa elimu ya juu, ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Kwa ujumla ni kwamba, fedha hizo zina mahitaji mengi ya muhimu kwa umma, ndiyo maana zikawekewa sheria ili vyama vifikie vigezo ndipo vipewe, vingine kila mmoja angeanzisha chama ili kujizolea ruzuku.

# Uhasama majimboni, 'miba njiani', corona vibano vilivyokwaza kinamama Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

LICHA ya vitisho vingi vinavyowatatiza wanawake kwenye kampeni kama mfumo dume, ukata mifukoni na hata uwepo wa maradhi ya corona kinamama Zanzibar hawakufanya ajizi, wamethibitisha uwezo wao kisiasa.

Ni Novemba 10, mwaka huu Baraza la 10 la Wawakilishi (BW), lilikutana katika kikao cha kikazi na kumchagua spika na naibu wake na kumpa jukumu la kuongoza mhimili huo wa dola Zubeir Ali Maulid na mwanamama Mgeni Hassan Juma jukumu la naibu.

Wawili hao wanakula kiapo cha utii kwa katiba ya Zanzibar, akiwa Naibu Spika Mgeni ni mwakilishi viti maalumu anayeingia barazani kupitia nafasi za wanawake wasomi. Katika historia ya Zanzibar anakuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi .

Anasema kuwa hata katika kugombea viti maalumu kama walivyo wanawake wengine , amepitia changamoto za kucheleweshwa na COVID -19 , ukosefu wa fedha lakini japo hakufika jimboni kuomba uwakilishi, ukweli unabaki kuwa matatizo yanayowakabili wanawake kwenye uwanja wa demokrasia za siasa hayana tofauti.

Mgeni anakipokea kijiti cha kuongoza vikao vya baraza kwa kuchaguliwa na kura zote za wajumbe 71 wa BW bila ya kupingwa ambapo anatetea nafasi yake hiyo kwa kipindi cha awamu ya pili na wajumbe wa baraza hilo wamemwamini kutokana na utendaji kazi wake tangu ngwe ya kwanza 2015.

Mgeni anaapishwa katika hafla iliyokuwa na msisimko wa aina yake hasa kwa wajumbe wageni ambao wameingia katika baraza hilo kwa mara ya kwanza baada ya kushinda uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Kina mama wengine walioshinda ubunge kwenye kipindi cha changamoto kadhaa ikiwamo corona ni Harusi Suleiman . Ni mmoja ya wawakilishi waliochaguliwa kwa mara ya pili kuwawakilisha wapiga kura wa jimbo la Wete Pemba kupitia CCM .

Mwanamama huyu aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya anasema ushindi wake haukuwa rahisi kwa sababu ya changamoto nyingi zinazowakabili wanawake lakini kubwa zaidi athari zilizosababishwa na COVID-19.

Harous anakiri ugonjwa huu ambao uliyakumba mataifa mengi duniani si tu uliwaathiri wanawake kiuchumi lakini pia ulikaribia kudidimiza matarajio yao kisiasa.

"Ilikuwa ni kipindi kigumu sana. Nilipoamua kuweka wazi azma yangu ya kugombea, Zanzibar ilikuwa inapambana na janga la COVID-19 na serikali ilikuwa imeweka mikakati ya kukabiliana na maradhi hayo ikiwamo kuzuia mikusanyiko ya watu ili kudhibiti kuenea kwa maambukizi," anasema.

Anaeleza kuwa ilikuwa vigumu kuwafikia watu, kila mmoja alikuwa amejifungia ndani na haikuwa rahisi kutembeleana, kila mmoja aliogopa kuambukizwa, hofu ya maradhi ya COVID-19 ilikuwa kubwa," anaongeza .

Hata hivyo, licha ya changamoto ya maradhi, hakutaka iwe kikwazo cha kukatisha ndoto yake ya kugombea nafasi ya uongozi katika vyombo vya kufanya uamuzi na kuanza kutumia simu yake kuwasiliana na watu wake wa karibu kuomba ushauri kuhusu uamuzi wake wa kuwa mwanasiasa pamoja na kubadilishana mawazo na wanachama wenzake ndani ya CCM huku akiwaomba wamuunge mkono.

Hatimaye, anasema alichukua fomu na hakufanya ajizi vikao vya juu vya chama vilimpitisha kuwa mgombea wa uwakilishi jimbo la Wete na ana mengi ya kusimulia akisema:

"Katika uliongo wa kisiasa kuna uhasama mkubwa hasa kwa wanawake. Njia ya kampeni ilikuwa imejaa miba kwa wanawake ambao wamedhulumiwa hako yao ya kutafuta na kuufikia uongozi. Lakini hali ilikuwa ngumu zaidi baada ya kuibuka kwa COVID-19. "

> "Wanawake walikuwa wakipambana kana kwamba hakuna kitu kilichotokea. Tulipata msaada mzuri kutoka asasi za kiraia kama Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) kuhusu namna bora ya kuwa...

"Kuna wanawake wenzetu walishindwa kuandaa mikutano ya kampeni kwa sababu hawakuna pesa. Walitarajia kupata pesa kutoka katika kazi za mikono na biashara, lakini haikuwezekana kwa sababu kila kitu kiliathiriwa na ugonjwa wa COVID-19," anakumbusha Harous.

Anasema changamoto kama hizi ndizo zinanazowafanya wanawake kutopata nafasi za uongozi kisiasa.

Kulingana na sensa ya watu na makazi, wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya idadi yote ya Wazanzibari lakini ni wachache waliomo kwenye vyombo vya uamuzi hali ambayo inawafanya wanaume kuamua kwa niaba yao.

Anasema licha ya changamoto za COVID-19, wanawake hawakukata tamaa badala yake waliendeleza mapambano kuhakikisha wanashinda vikwazo vilivyoletwa na ugonjwa huo na changamoto nyingine za kiuchumi.

"Idadi yetu katika vyombo vya uamuzi itakuwa kubwa kuliko hapo awali. Wengi wetu tumeshinda majimboni na pia tumepata viti zaidi katika uteuzi na viti maalum vya wanawake. Ndani ya CCM kuna wanawake 18 walioteuliwa kwa viti maalum na watatu hadi sasa waliteuliwa kwa nafasi ya urais, "anasema.

"Wanawake walikuwa wakipambana kana kwamba hakuna kitu kilichotokea. Tulipata msaada mzuri kutoka asasi za kiraia kama Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) kuhusu namna bora ya kuwa mwanasiasa,'anasema Asha Abdallah Mussa, mwakilishi wa jimbo la Mahonda.

Anawahimiza wanawake kujifunza kutoka kwa wengine ambao wamejaribu na kufanikiwa, akisema kwamba wakati ujao, mitazamo finyu juu ya wanawake, mfumo dume, mila na changamoto zingine zitashindwa.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk Mzuri Issa, anasema mbali ya kuwapongeza wanawake walioiboa kisiasa anakiri kwamba ugonjwa wa COVID-19 ulileta changamoto sio tu kwa wanawake ila jamii nzima kwa ujumla.

Anasema TAMWA ikishirikiana na wadau wake kama UN-Women iliwafikia zaidi ya wanawake 1,000 kuwapa elimu ya uongozi na kuwandaa kuwa wanasiasa katika uchaguzi mkuu uliomalizika karibuni.



Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid , akimwapisha Mgeni Hassan Juma, kuwa Naibu Spika. Ni katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

UCHAGUZI UMEKWISHA....

# Ni dhana inayowahusu wote waliopigiwa na wapigakura



Rais John Magufuli, akizindua na kuhutubia bunge wiki iliyopita jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Peter Mabiki**

"Uchaguzi umekwisha sasa tufanye kazi". Ni kauli ilitolewa na Rais John Magufuli siku alipopewa cheti cha ushindi wa matokeo ya uchaguzi mkuu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kingine tena cha miaka mitano.

Ni dhahiri kwamba uchaguzi umekwisha sasa kinachotarajiwa na wananchi kutoka kwa viongozi wao ni kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya wapigakura wote.

Kipindi cha uchaguzi ni muda wa kufanya siasa za majukwaani, kila mgombea kutoa sera zake na kutangaza ilani ili apate nafasi ya kuchaguliwa kuongoza nchi ama jimbo. Uchaguzi unapokwisha viongozi walioteuliwa wanatakiwa kuanza kufanya kazi kwaajili ya maendeleo ya wananchi wao.

Matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa kuanzia Novemba 28, 2020 yanaonyesha kuwa kuna mambo ambayo Watanzania wanatarajia kuyaona kutoka kwa viongozi wao, baadhi ya yale wanayoyahitaji ni pamoja na utekelezaji wa sera walizonadi kipindi cha kampeni, Watanzania wote pasipo kujali vyama vyao ama makabila yao wanatarajia kuona mambo yaliyonadiwa kwenye kampeni na viongozi hao zikitimizwa. Mtanzania alitoa kura kwa mgombea fulani kwa kuwa aliziamini sera alizozisikia kutoka kwa mgombea. Hivyo kila aliyepigakura atavunjika moyo pale mgombea huyo atakaposhindwa kutekeleza sera zake kama alivyoahidi.

Ni matarajio ya kila Mtanzania kwamba viongozi wote waliopata ushindi watatekeleza majukumu yao kwa manufaa ya wananchi waliowachagua na kutokana na sera walizoziahidi kipindi cha kampeni ikiwamo kile walichokieleza kwenye ilani za uchaguzi.

Pia Watanzania wanatarajia kwamba wabunge wao watawasilisha hoja na kero zao wawapo bungeni ili ziweze kutatuliwa kwa kuwahakikishia huduma bora za kijamii kama maji safi na salama, hospitali zenye wataalamu na vifaa tiba, shule za sekondari na msingi zenye walimu, vifaa na elimu bora.

> Kufanya kazi kwa bidii ni moja ya jukumu kubwa pia, Watanzania wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii. Itakumbukwa kuwa hii ni ngwe ya pili baada ya Tanzania kuingia katika uchumi wa kati. Hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa bidi. Ili uchumi wa mtu mmoja mmoja uweze kulandana na wa taifa ambao ni wa kiwango cha kati .

Haikuwa matarajio ya Mtanzania kumchagua mbunge ambaye akifika bungeni hazungumzi bali kazi yake inakuwa ni kusubiria kikao cha bunge kumalizika ili apokee stahiki zake mwisho wa kikao. Ni matarajio yao kwamba kila aliyepata dhamana ya kuingia bungeni atatambua jukumu lake na kwamba anajua kuwa kazi yake bungeni ni kutatua kero na matatizo ya wananchi wake.

Sasa umefika muda kila mbunge kuyapa uzito matatizo ya wananchi wake kama vile ambavyo anashughulika na matatizo ya familia yake ama yake binafsi. Itawapendeza wananchi kama jambo hili litatokea.

Ni imani ya wapigakura kuwa hakuna mwananchi ambaye anaweza kukata mti wa tunda alipendalo. Kwakuwa Watanzania wamemchagua mbunge wao hii inamaanisha kuwa mchaguliwa ni tunda la mti waupendao, hivyo ni muda mwafaka kuonyesha uwezo wako wa kuzaa matunda.

Imezoeleka kwamba wabunge wengi baada ya uchaguzi husahau kuwa Watanzania wamewapa mamlaka ya kutatua kero na matatizo ya wananchi katika majimbo yao kwa kuwazungumzia ndani ya bunge, kufuatilia kwenye taasisi na mashirika ya umma pamoja na wadau wengine.

Kwa hiyo umefika muda wabunge kufahamu na kuanza kutekeleza wajibu wao katika kuleta maendeleo jimboni kwao na kuachana na fikra kuwa hawana kipingamizi.

Wabunge waliochaguliwa watumie muda wao mwingi kukaa majimboni kwao ili kujua matatizo na kero za wananchi wao. Hii itasaidia kupata nafasi ya kuzijua kero na matatizo ya wapiga kura wake. Hii ndiyo maana halisi ya nuu uchaguzi umekwisha sasa tufanye kazi.

Mbali na viongozi, wananchi tuna wajibu gani baada ya uchaguzi kufikia tamati? Moja, kuendeleza amani ya nchi hii ambayo ni moja ya tunu za taifa. Inafahamika kwamba pasipo na amani hakuna maendeleo. Ni jukumu la kila mwananchi kuilinda amani ya nchi hii.

Watanzania wana wajibu wa kuilinda amani yao kama mboni za macho yao hatupaswi kuruhusu upenyo au mwanya wowote utakaofanya amani yetu kutoweka.

Kufanya kazi kwa bidii ni moja ya jukumu kubwa pia, Watanzania wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii. Itakumbukwa kuwa hii ni ngwe ya pili baada ya Tanzania kuingia katika uchumi wa kati. Hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa bidi. Ili uchumi wa mtu mmoja mmoja uweze kulandana na wa taifa ambao ni wa kiwango cha kati .

Hivyo inahitaji kufanya kazi kwa bidii, kuchangia maendeleo ya nchi na pia kupata kipato kwa ajili ya kulipa kodi ambayo ni mapato ya serikali kuleta maendeleo kwa wananchi.

Nafsi ya Mtanzania siyo kulalamika kwamba serikali haijafanya hiki ama kile bali ni kuanza kuangalia ni kipi utaweza kufanya kwa ajili ya maendeleo yako pamoja na nchi yako. Rais wa Marekani John F. Kennedy (JFK) aliwahi kusema: "Ask not what your country can do for you–ask what you can do for your country."

Kendedy alimaanisha kwamba usiulize nchi yako imekufanyia nini, bali uliza wewe umeifanyia nini nchi yako kwa vile nawe una mchango wa kuitumikia Tanzania, anza kujiuliza sasa.

Mwisho, itoshe kusema kwamba ni kweli uchaguzi umefikia tamati Rais, wabunge na madiwani wamekwisha patikana. Serikali itaundwa na bunge litaundwa kilichobaki kwa wananchi pamoja na viongozi ni kufanya kazi. Kila Mtanzania achape kazi ili tuweze kujenga nchi yetu kwa umoja wetu. Kila Mtanzania ajiulize utafanya nini kwa ajili yako na nchi yako.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika Mashariki, Mungu Ibariki Afrika.**

**Kwa maoni na ushauri**
**+255767664608**
**+255683660808**
**petermabiki.pm@gmail.com**
**Arusha, Tanzania.**

# BURIANI JENERALI RAWLINGS GWIJI LA UKIMWI AFRIKA

## •ALIZINDUA TACAIDS DODOMA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa zamani wa Ghana, Jerry Rawlings, aliyeaga dunia wiki iliyopita anatajwa kwa mengi. Mojawapo ni kuwa ofisa wa juu wa kikosi cha anga cha Ghana, aliyeongoza mapinduzi mara mbili, akijaribu mwaka 1979 lakini cha ajabu baada ya kupindua , akakabidhi madaraka kwa serikali ya kiraia.

Hata hivyo hakupoa baada ya miaka miwili alifanya tena mapinduzi na kuhakikisha kuwa waliokuwa wanatuhumiwa kwa ubadhirifu wanashughulikiwa.

Aliiongoza Ghana kama kiongozi wa jeshi hadi uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1992, alipokuwa rais wa kwanza mteule na kuondoka madarakani mwaka 2001 baada ya kuhudumu kwa mihula miwili ikulu.

Rawlings au mtu mwenye haiba, aliingia madarakani 1979 akipambana na ufisadi akiwa na agenda ya kupambana na wizi wa mali ya umma ya Ghana na uongozi mbaya.

Kifo cha kiongozi huyo wa zamani kinaelezwa kuwa kilitokea katika hospitali moja jijini Accra, baada ya kuugua kwa muda mfupi kikihusishwa na COVID- 19, Ijumaa Novemba 12, akiwa na miaka 73.

**ADHABU YA KIFO**

Rais huyo mwenye asili ya Scotland, anakotoka baba yake wakati mama alikuwa Mghana, anaelezwa kuwa katika miezi michache ambayo alichukua uongozi wa nchi hiyo mwaka 1979, alikuwa na jukumu la kutekeleza adhabu ya kifo dhidi ya wakuu kadhaa wa zamani wa serikali na majenerali wa jeshi kwa madai ya ufisadi na usimamizi mbaya wa mali za umma.

Aliunda kikosi cha kijeshi cha mauaji kilichoua kwa maelekezo ya ikulu, huku akielezwa kuwa alionekana kama mwokozi wa maskini kwani alitumia muda wake madarakani kama mjamaa aliyejitolea.

**ALINYONGA MARAIS 3**

Anadaiwa kuwaua marais watatu akiwamo Ignatius Kutu Acheampong, aliyekuwa kiongozi wa mapinduzi ya kijeshi nchi humo aliyeuawa na kikosi maalumu cha kuua kilichoundwa na Rawling baada ya kuiongoza Ghana kuanzia Januari 1972 hadi Julai 1978, alipopinduliwa.

Maraisi wengine ni Luteni Jenerali Frederick W. K. Akuffo na Luteni Jenerali Akwasi Amankwaa Afrifa, aliyekuwa askari, kiongozi wa jadi na Rais wa Ghana akiongoza kijeshi mwaka 1969 hadi 1970.

Rawlings anasifika kuwa baadaye alianzisha mageuzi ya soko huria na akaanzisha kipindi kirefu cha utulivu wa kisiasa, ambao unaendelea hadi leo, baada ya msururu wa mapinduzi katika miaka ya 1960 na 1970.



Jenerali Jerry Rawlings akifurahia ushindi wa chama chake baada ya kuanzisha siasa za vyama vingi. **PICHA: MTANDAO.**

**KUVUA GWANDA**

Kati ya mwaka 1983 na 1987, Rawlings alijaribiwa mara kadhaa kupinduliwa na kunusurika kupinduliwa ya kijeshi. Hata hivyo, Ghana ilipitia kipindi kichungu cha hali ngumu ya uchumi na kiongozi huyo aliyekuwa bingwa wa kukosoa na kuhukumu kifo alilazimika kuomba msaada kwenye Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

IMF iliisaidia Ghana kuimarisha uchumi wake kupitia sera za mageuzi na kufufua uchumi na mwishoni taifa hili liliachana na uongozi wa kijeshi na mapinduzi na kuingia kwenye utawala wa kiraia na siasa za vyama vingi.

Mwaka 1992, aliunda Tume ya Katiba ya Ghana iliyoshughulikia uundwaji wa katiba iliyowezesha kuundwa kwa serikali ya kiraia na kuwa moja ya nchi za Afrika zenye katiba bora.

Rawlings aliunda chama kipya cha kisiasa cha National Democratic Congress (NDC) ambacho kilishinda uchaguzi mkuu mwaka 1992 .

Kiongozi huyo alishinda uchaguzi mkuu 1992 na ule wa 1996 na kuachana na magwanda ya kijeshi akivaa vazi la kitenge la nchi hiyo lililopewa jina la 'kente'.

> Ujio wa Rawlings ulitangazwa na Ofisi za Umoja wa Mataifa jijini Dar es Salaam zilieleza kuwa kiongozi huyo akiwa nchini kuanzia Novemba mosi hadi tano angehamasisha zaidi kuhusu kupambana UKIMWI ambao Mkapa aliutangaza rasmi kuwa ni janga la kitaifa.

Kuanzia hapo akawa akitaniwa kutoka gwanda la khaki hadi kente. Ikimaanisha kuondoka kwenye uongozi wa kijeshi na kuingia kwenye mavazi ya uraiani.

Baada ya kujaribu kuirudisha Ghana kwenye mstari kuanzia kwenye jeshi hadi uraiani, Rawlings alikabidhi nchi yake kwenye uongozi wa kiraia ulioongozwa na Rais wa kiraia Dk Hilla Limann.

**TANZANIA INAVYOMKUMBUKA**

Kiongozi huyo wa zamani wa Ghana aliyekuwa pia 'voluntia' wa Shirika la UKIMWI la Umoja wa Mataifa (UNAIDS) anakumbukwa kwa kuzindua Tume ya Taifa ya Ukimwi (TACAIDS).

Wakati huo ikiongozwa na Mwenyekiti Meja Jenerali Herman Lupogo, TACAIDS ilihitaji kufanyakazi na wabunge ikishirikiana na Kamati ya Bunge ya UKIMWI, iliyokuwa ikiongozwa na Mwenyekiti Lediana Mung'ong'o.

Alifanyakazi hiyo mkoani Dodoma na kulihutubia Bunge mwaka 2000 ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya siku tano nchini wakati huo mwenyeji wake akiwa ni Rais Benjamin Mkapa.

Ujio wa Rawlings ulitangazwa na Ofisi za Umoja wa Mataifa jijini Dar es Salaam zilieleza kuwa kiongozi huyo akiwa nchini kuanzia Novemba mosi hadi tano angehamasisha zaidi kuhusu kupambana UKIMWI ambao Mkapa aliutangaza rasmi kuwa ni janga la kitaifa.

Rawlings wakati huo alikuwa ni miongoni mwa watu mashuhuri barani Afrika anakumbukwa pia katika hamasa za kupambana na UKIMWI Zanzibar na katika ziara yake alikutana pia na Rais Aman Abeid Karume wa Zanzibar.

Aidha kazi yake ya kuwashwa moto wa vita ya UKIMWI Tanzania ilimkutanisha pia na asasi za kiraia, wafanyakazi wa mashirika ya UN, 'voluntia' pia jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Kinara huyo wa UN wa kupambana na UKIMWI alizizuru pia Kenya na Ethiopia katika jitihada za kuhamasisha vita dhidi ya UKWIMI.

**MITANDAO**



# Wazazi/ walezi waonywa kuamini mila potofu

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WAZAZI na walezi wa watoto wenye ulemavu wameshauriwa kuachana na mila potofu ya kuwaona kuwa ni sehemu ya mikosi kwenye familia zao na kuwanyima haki zao za msingi.

Ushauri huo, ulitolewa jana na mwezeshaji wa elimu jumuishi kuhusu ulemavu na watu wenye ulemavu, Wilaya ya Dodoma na Bahi, Fortunatus Raphael, alipokuwa akitoa mafunzo kwa asasi za kiraia kuhusu ushawishi na utetezi.

Alisema, imani potofu ni sababu ya watoto wenye ulemavu kushindwa kupatiwa haki zao za msingi kwa kuwaona ni mkosi.

Alisema kuna makundi makubwa ya watoto wenye ulemavu wanaofichwa nyumbani, badala ya kwenda shule.

Awali, wanafunzi wa Shule ya Msingi Ibihwa wilayani Bahi, waliiomba serikali kuchukua hatua za kisheria kwa wazazi na walezi wanaozima ndoto ya kujikomboa na umaskini kwa mtoto mwenye ulemavu.

Andrea Ladislai (15), alisema bado kuna ukandamizaji kwa watoto wenye ulemavu wanaofanyiwa na wazazi, walezi na hata jamii kuwaona hawastahili kupatiwa haki zao za msingi kama ilivyo kwa wengine.

"Sisi watoto wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma tunaiomba serikali kuliangalia suala hilo la ukandamizaji wanaofanyiwa watoto wenzetu wenye ulemavu ambao wanazimishwa ndoto ya kujikomboa na umaskini walionao," alisema.

Mratibu wa elimu jumuishi Wilaya ya Bahi na Dodoma kutoka kanisa la Free Pentecost Church of Tanzania, Jane Mgidange, alisema kuwa bado kuna majengo ya serikali yasiyo rafiki kwa watu wenye ulemavu hali inayoonyesha unyimaji wa haki zao kwa kundi hilo.

# Tanzania yapata soko mahindi ya njano Misri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imepata soko la mahindi ya njano nchini Misri, huku tani milioni moja zikihitajika kwa mwaka.

Mahindi hayo yataanza kuuzwa kuanzia mwezi Julai mwaka 2021 kupitia kampuni ya Smart Group ya Misri.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao alichofanya na Mwenyekiti wa kampuni ya Smart Group, Yasser Attia, aliyetembelea Tanzania kutafuta masoko ya mazao ya nafaka.

Kusaya alisema wizara hiyo kwa ushirikiano na ofisi ya ubalozi wa Tanzania nchini Misri imefanikiwa kuwashawishi wafanyabiashara hao kuja Tanzania kuona na kujadili fursa za masoko ya wakulima, ili kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao.

**Tumekuja Tanzania tukiamini ni ndugu zetu tunategemea kuongeza uhusiano wa kibiashara ili wakulima wa mahindi wazalishe zaidi na kupata faida kupitia ushirikiano huu na Misri.**

"Kampuni ya Smart Group toka Misri imekubali kununua mahindi ya njano tani milioni moja toka kwa wakulima wa Tanzania kuanzia mwezi Julai 2021 kufuatia mazungumzo yetu leo hapa Dodoma," alisema.

Alisema mahindi ya njano yanayotakiwa na kampuni hiyo ni kwa ajili ya matumizi ya kuzalisha chakula cha mifugo na samaki, ikiwa ni fursa kwa soko la Tanzania kwa kuwa Watanzania wengi hawali mahindi ya njano.

Kusaya alisema kwa sasa uzalishaji wa mahindi ya njano nchini ni mdogo hatua ambayo itakuwa ni fursa kwa wakulima kuongeza uzalishaji wa mahindi hayo.

"Uhalisia uliopo sasa ni kuwa uzalishaji wa mahindi ya njano ni mdogo kutokana na Watanzania wengi kutotumia mahindi haya kama chakula, hivyo kufuatia makubaliano tutakayoingia na Smart Group tutahamasisha wakulima kuanzia msimu huu Novemba walime kwa wingi kwa kuwa soko limepatikana," alisema Kusaya.

Kwa upande wake, Attia alisema Misri inahitaji mahindi ya njano tani milioni nane kwa mwaka ambayo kwa sasa zaidi wanaagiza kutoka Argentina na Ukraine.

Alisema mwelekeo wa Serikali ya Misri chini ya Rais Abdel Fattah el-Sisi ni kuona nchi hiyo inawekeza zaidi kwenye mataifa ya Afrika ndio sababu ya kuja Tanzania kutafuta soko la mazao.

"Tumekuja Tanzania tukiamini ni ndugu zetu tunategemea kuongeza uhusiano wa kibiashara ili wakulima wa mahindi wazalishe zaidi na kupata faida kupitia ushirikiano huu na Misri," alisema Attia.

Attia aliongeza kuwa nchi ya Misri ina uhitaji wa mazao mengi ya kilimo yakiwamo matunda kama parachichi, nanasi, papai, viungo, kahawa, korosho na chai na kwamba wataangalia ubora na gharama za usafirishaji mazao hayo kutoka Tanzania hadi Misri kwa njia ya bandari ili waingie mikataba ya ushirikiano kwenye biashara.



Vijana waliomaliza elimu ya vyuo mbalimbali wakiangalia majina yao kwenye orodha iliyobandikwa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bahi, mkoani Dodoma jana, kwa ajili ya nafasi zilizotolewa za maofisa watendaji wa vijiji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaombwa kurekebisha sheria ya usalama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 ili kupunguza ajali.

Akizungumza jana jijini hapa katika maadhimisho ya kumbukumbu ya waathirika wa ajali za barabarani nchini, Mwenyekiti wa Chama cha Wanasheria Kanda ya Dodoma (TLS), Marry Mushi, alisema anaamini Bunge la 12 litafanyia marekebisho sheria hiyo kwa kuwa tayari walishawasilisha mapendekezo serikalini.

Alisema, Bara la Afrika linaongoza kwa ajali nyingi za barabarani licha ya kuwa ina magari kwa asilimia mbili ambazo zinagharimu maisha ya watu.

"Takwimu zinaonyesha kuwa nchi za Afrika zinaongoza kwa kuwa na ajali nyingi za barabarani duniani kuliko mabara mengine," alisema Mushi.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa watu milioni 1.35 hufariki dunia kila mwaka Afrika kutokana na ajali za barabarani na kusababisha kuathiri uchumi wa nchi.

"Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kimeandaa kumbukumbu hii ili kupinga ajali za barabarani ikiwa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kuzuia na athari za ajali hizo," alisema Mushi.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Dodoma, Prakson Rugazia, alisema kwa upande wa Tanzania vidhibiti mwendo vimesaidia kupunguza ajali za barabarani.

"Hivi sasa ajali za barabarani hapa Tanzania zimepungua sana na hii ni kutokana na vidhibiti mwendo ambavyo vimefungwa katika mabasi ya abiria na baadhi ya magari," alisema Rugazia.

Pia alisema baadhi ya adhabu zimeongezeka pamoja na elimu inayotolewa na jeshi hilo kupitia vyombo vya habari, nyumba za ibada na vijiwe vya bodaboda.

Rugazia alisema ajali hizo zinasababishwa upungufu unaotokana na makosa ya kibinadamu ambayo yapo kwa asilimia sita, ubovu wa vyombo vya usafiri, asilimia 16 na hali ya ubovu wa miundombinu asilimia 18.

Alisema hivi sasa watu wanatengeneza magari yao hali inayochangia pia kupunguza ajali.



# Misaada yazidi kumiminika aliyejifungua watoto wanne

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MISAADA imeendelea kumiminika kwa Stella Kalinda (34), mkazi wa Kijiji cha Idendeluka, Chunya mkoani Mbeya ambaye alijifungua mapacha wanne wiki iliyopita.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, ndiyo iliyoongoza wadau mbalimbali kutoa misaada hiyo kwa kutoa Sh. 185,000 ambazo zilikabidhiwa kwa familia ya mwanamke huyo kusaidia malezi ya watoto hao.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, Mayeka Simon, aliwaomba wadau wengine hata ambao wako nje ya wilaya kujitokeza kumsaidia mama huyo kwa kuwa malezi ya watoto hao ni magumu.

Mayeka alisema familia ya mwanamke huyo ina uchumi wa kawaida na inategemea kilimo na uchimbaji mdogo, hivyo malezi ya watoto hao yanahitaji msaada wa wadau.

**Misaada inayohitajika ni fedha, mavazi na chakula kwa ajili ya mama huyo, ili aendelee kuwahudumia watoto wake ambao mpaka sasa bado yuko nao hospitalini.**

"Nawapongeza sana madaktari waliomhudumia mama huyu pamoja na watoto wake. Lakini ninachowaomba Watanzania wenzangu ni kuendelea kuonyesha upendo kwa mama huyu kwa kumsaidia kwenye malezi," alisema Mayeka.

Alisema misaada inayohitajika ni fedha, mavazi na chakula kwa ajili ya mama huyo, ili aendelee kuwahudumia watoto wake ambao mpaka sasa bado yuko nao hospitalini.

Baadhi ya wadau waliojitokeza kutoa msaada ni mfanyabiashara Ayubu Omary, kampuni mbalimbali za wachimbaji na watu binafsi ambao walitoa fedha taslimu na nguo za kuwasitiri watoto.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Dk. Felister Kisandu, alisema mama huyo alijifungua watoto alfajiri ya Novemba 10, mwaka huu, katika Kituo cha Afya cha Chalangwa.

Alisema kati ya watoto hao wanne ni mmoja pekee ndiyo wa kike na kwamba wamezaliwa wakiwa na afya njema na uzito wa kawaida tofauti na ambavyo huwa inatokea kwa mapacha wengine wanaozaliwa wengi.

Dk. Kisandu alisema kati ya watoto hao, wawili ambao ni mmoja wa kike na mwingine wa kiume walizaliwa na kilo mbili kila mmoja, huku wawili wengine wakiwa na uzito tofauti, mmoja kilo 2.9 na mwingine kilo 2.7.

"Baada ya kupata taarifa za mama huyo kujifungua kwenye hicho kituo, tulituma gari kwenda kuwachukua na kuwaleta hapa. Tuliwaweka kwenye chumba cha uangalizi maalumu yaani NICU (Neonatal Intensive Care Unit)," alisema Kisandu.

Akizungumza na waandishi wa habari hospitalini hapo, mama huyo alisema uzao wa watoto hao ni wa sita na kwamba wengine watano alikuwa anajifungua mmoja mmoja.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kumsaidia kwa maelezo kuwa hali yake ya maisha ni ngumu na hana uchumi wa kumwezesha kuwalea watoto wake.



Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Yohana Nguluka, akitoa maelezo kuhusu uhifadhi wa vyanzo vya maji, wakati wa kikao cha wadau wa bonde la Ziwa Rukwa kilichofanyika wilayani humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TARI Uyole yaanza mfumo sokoni, shambani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, imeanza kufanya utafiti kwa kuanzia sokoni kabla ya kwenda shambani, ili wanapozalisha teknolojia mpya ziwe zinazingatia mahitaji ya soko la mazao ya wakulima.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema jana hayo kwenye kikao cha tathmini ya utafiti wa kilimo kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita kilichofanyika jijini Mbeya.

Alisema wameamua kuanzisha utaratibu wa kuanzia sokoni kwa kuzingatia mahitaji ya bidhaa zinazohitajika na kuzalisha teknolojia ambazo zitapelekwa kwa wakulima ili kukidhi mahitaji.

"Kwa sasa tafiti (utafiti) zetu (wetu) za (wa) teknolojia zimelenga (umelenga) masoko kwanza ili kujua mahitaji ya walaji hivyo fomula yetu itakuwa sokoni- shambani na kisha sokoni tena," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kuwa TARI Uyole imebuni teknolojia 15 kwa ajili ya kilimo na kwamba zimelenga kuongeza tija ya uzalishaji kwa mkulima ikiwamo ya uhandisi wa kilimo ambayo inasaidia kurahisisha shughuli za kilimo, afya ya udongo kupima na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuhifadhi na kutibu, teknolojia ya kupambana na visumbufu, mimea na wadudu pamoja na uhaulishaji wa teknolojia kwa kutumia mashamba darasa na vyombo vya habari.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Saitoti Zelothe, alisema watafiti wa kilimo wanapaswa kutambua kuwa wanadhamana kubwa katika kuendeleza maisha ya Watanzania.

# Wazawa Mbeya wachangia maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa watu mbalimbali waliozaliwa, kuishi na kufanya kazi mkoani Mbeya, maarufu kama Mbeya Family Group (MFG), umeanza mikakati ya kuboresha huduma za kijamii hasa elimu na afya kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Michael Mwangoka, alisema jana kwamba umoja huo ulianzishwa mwaka 2019 na una zaidi ya wanachama 150 ambao wanaishi ndani na nje ya nchi.

Alisema wameanza kuboresha huduma za kijamii kwa kuanzia katika Shule ya Msingi Majengo ya jijini Mbeya kwa kukarabati vyoo vyenye matundu 12 kwa ajili ya wanafunzi na kwamba wanaendelea na mchakato wa kuzifikia shule zingine.

Mwangoka alisema mbali na shule hiyo, pia walitoa msaada wa chakula na vifaa vya shule kwa watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto yatima vya Simike na Soweto.

"Ni jukumu letu sisi kuubadilisha mkoa wetu na kuufanya uwe na maendeleo kama mikoa mingine, tutaendelea kusaidia kukarabati vyoo kwenye shule zetu na majengo ya maeneo mengine ambayo ni muhimu zikiwamo hospitali zetu," alisema Mwangoka.

Aliwataka watu wengine ambao wamezaliwa, kusoma, kufanya kazi na wana mapenzi mema na Mkoa wa Mbeya, kujiunga na umoja huo ili kuendelea kushirikiana na serikali kwenye uboreshaji wa huduma za kijamii.

Naye Jaji mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Atuganile Ngwala, ambaye ni mwanachama wa umoja huo, alisema Jiji la Mbeya kwa sasa halina hadhi ya kuwa Jiji kutokana na mazingira yalivyoharibika.

Alisema jiji hilo halina barabara nzuri, halina makazi yaliyopangiliwa kama ilivyokuwa mwanzo wakati kata za Majengo, Ghana na Maendeleo zilivyokuwa zimepangwa ingawa kwa sasa anadai barabara zake zimeharibika na majengo hayajaboreshwa.

Jaji Ngwala alisema kwa sasa kila mdau anatakiwa kuchukua hatua ya kuhakikisha anashirikiana na serikali kwenye uboreshaji wa Jiji hilo, ili liendane na hadhi ya jina ambalo lilibatizwa la Jiji la Kijani (Green City).

"Huu si wakati wa kuisubiri Halmashauri ya Jiji au Serikali Kuu kuboresha huduma za kijamii kama afya, elimu na mazingira bali tunatakiwa kujitolea kwa pamoja ili tuharakishe maendeleo," alisema Jaji Ngwala.

Naye mwalimu mstaafu wa Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Sangu, Simon Makandi, aliwashauri wanachama wa umoja huo, kuunda taasisi ambayo itakuwa inajishughulisha na shughuli za uzalishaji mali badala ya kutegemea michango pekee.

Alisema endapo taasisi hiyo itaundwa, itakuwa rahisi kutekeleza malengo yao na hata kuaminiwa na wadau na hata kusaidia wanachama wake kupata ajira.

Alizitaja baadhi ya shughuli ambazo taasisi hiyo inaweza kuzifanya kuwa ni pamoja na kilimo, ufugaji na uvuvi huku akisisitiza kuwa ndizo shughuli ambazo zinaweza zikawapa jeuri ya kutekeleza kwa ufasaha miradi wanayokusudia kuitekeleza.





# Kampuni yaonyesha nia uwekezaji miradi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa kampuni ya kimataifa ya Arena, yenye makao makuu nchini Ujerumani inayojishughulisha na miradi ya uwekezaji katika sekta ya nishati ya umeme, imeonyesha nia ya kutaka kuwekeza miradi yake visiwani Zanzibar baada ya kuridhika na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Mwakilishi wa kampuni hiyo, Souheil Freich, aliyeambatana na uongozi wa kampuni ya Flagfin yenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, Vuga Mjini hapa.

Freich alisema alikuwa akifuatilia harakati za sera na ilani za uchaguzi mkuu uliopita na kuridhika nazo kitendo kilichoipa ushawishi kampuni yake kutaka kuitumia nafasi ya uwekezaji ndani ya ardhi ya Tanzania.

Alisema uwapo wake umemthibitishia kwamba mazingira ya uwekezaji Tanzania Bara na Zanzibar yanastahiki kutumiwa na wawekezaji wenye nia thabiti ya kutaka kuzisaidia jamii katika maeneo husika kulingana na miradi itakayoanzishwa.

Alimweleza Hemed kwamba taasisi yake ya uwekezaji imeshabobea katika fani ya uwekezaji kwenye masuala ya nishati ya umeme wa jua pamoja na taaluma ya utengenezaji wa mbolea ambayo inaweza kuifaidisha Zanzibar endapo itapata fursa ya kutoa mchango wake.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdalla, alisema ujio wa wawekezaji tofauti nchini ni ishara ya kuunga mkono kasi ya serikali katika mipango yake ya kuimarisha uchumi.

Hemed aliuhakikishia uongozi huo kwamba Serikali ya Zanzibar inahitaji utaratibu na sheria kuona wawekezaji hao wanakamilisha maombi yao kwa vile hakutakuwa na ubabaishaji ili kasi ya uwekezaji iimarike zaidi kwa kuondoa urasimu.

Alisema wapo baadhi ya wawekezaji waliowahi kuonyesha nia ya kutaka kuwekeza miradi yao nchini, lakini wakakata tamaa baada ya usumbufu walioupata uliosababishwa na ubinafsi wa baadhi ya watendaji wa taasisi za umma.

# Mwili wa askari aliyeuawa wapatikana ukiwa umefukiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWILI wa askari wa Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ), Khalfan Junedi (25), aliyedaiwa kuuawa na watu wasiojulikana kisiwani Pemba hatimaye umepatikana.

Askari huyo alipotea katika mazingira ya kutatanisha akiwa katika doria kipindi cha uchaguzi mkuu eneo la Ngwachani, Wilaya ya Mkoani, Pemba.

Alipotea akiwa na bunduki aina ya AK47 ikiwa na risasi 21 ambayo imepatikana.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Ahmed Khamis Makarani, alisema mwili huo ulipatikana katika Kijiji cha Chonga kwenye bonde la Kisitu-Mbwa.

Alisema, Novemba 15 walifanikiwa kuupata mwili wa askari huyo baada ya kumkamata Ussi Foum Machano, mkazi wa Ngwachani, ambaye aliwapeleka kwenye eneo alilofukiwa.

"Novemba 12, tulimkamata Ussi eneo la Chakechake ambaye tulimhoji na akatuambia mahala ilipo bunduki na baadaye kwenda kutuonyesha eneo ulipowekwa mwili wa marehemu huyo," alisema Kamanda Makarani.

**Wananchi wa Kijiji cha Ngwachani waliopata taharuki na kukimbia kwa kuogopa msako ambao ulifanywa na vikosi, warudi katika maeneo yao, sisi tutaendelea kufanya upelelezi wa kisayansi zaidi.**

Alisema, baada ya kufanyiwa uchunguzi, walibaini kuwa marehemu kabla ya kifo chake, alikuwa na majeraha ya kupigwa mwilini mwake, huku akiwa amekatwa baadhi ya viungo.

"Taratibu zote za kiuchunguzi kuhusiana na mwili zimefanywa baadaye, mwili huo umesafirishwa kwenda Unguja kwa ajili ya mazishi," alisema.

Alisema, upelelezi wa kesi hiyo unaendelea na watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika na wanaendelea kuwasaka wahusika wengine wa tukio hilo.

Alisema, Oktoba 28, mwaka huu askari huyo pamoja na wengine walikuwa kwenye doria za kawaida, alipotea majira ya saa 2:00 usiku huku akiwa na bunduki ya AK47.

"Baada ya kupotea, polisi, vyombo vya ulinzi na wananchi waliendelea kufuatilia taarifa za kupotea kwake," alisema.

Kamanda Makarani, aliwataka wananchi wa Ngwachani kurudi katika maeneo yao wanayoishi, ili waendelee na shughuli zao za kimaisha, kwa kuwa hali ya amani na utulivu imerejea.

"Waliokuwapo maporini warudi na waliokuwapo nje ya Pemba warudi, sisi kimsingi tunawatafuta watu ambao kwa namna moja ama nyingine, wamehusika na mauaji ya huyo askari na sio wananchi wa kawaida," alifafanua.

Naye Mkuu wa Upelelezi Mkoa Kusini Pemba, Richard Tadei Mchomvu, aliwasihi wananchi waliokimbia kwa kuogopa msako, warudi ili waendelee na shughuli zao kiuchumi na kuwataka wanafunzi warudi kuendelea na masomo.

"Wananchi wa Kijiji cha Ngwachani waliopata taharuki na kukimbia kwa kuogopa msako ambao ulifanywa na vikosi, warudi katika maeneo yao, sisi tutaendelea kufanya upelelezi wa kisayansi zaidi," alisema.

Aliwashauri wanaohisi kutajwa na huku wakijua kuwa hawahusiki na tukio hilo, wafike kituo cha polisi kujisalimisha mwenyewe, huku akiwaomba wananchi kuzidisha ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kuwabaini waliohusika na tukio hilo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah (kulia), akizungumza na mwakilishi wa kampuni ya kimataifa Arena ya Ujerumani inayojishughulisha na miradi ya uwekezaji katika sekta ya nishati ya umeme, Souheil Freich, alipomtembelea ofisini kwake, mjini Zanzibar jana, kuwasilisha nia yake ya kutaka kuwekeza nchini. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Atoa siku 3 vibanda biashara viondolewe kituoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib Hassan, ametoa siku tatu kwa uongozi wa Jiji la Zanzibar, Wilaya ya Mjini na Baraza la Manispaa Mjini, kuondoa vibanda vya biashara katika eneo la Kijangwani katika eneo la kituo cha daladala.

Alitoa agizo hilo jana, wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika eneo hilo na mengine ya Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharbi B akiwa na viongozi, watendaji na wafanyakazi wa taasisi hizo.

Aliwaeleza kuwa eneo hilo waliwekwa wafanyabiashara kwa dharura wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona lengo likiwa kupunguza msongamano wa watu katika masoko mengine na kuwataka wawahamishie wafanyabiashara hao katika eneo jingine walilowapangia ili kuruhusu eneo hilo kutumika kwa shughuli iliyokusudiwa.

Aliwaambia viongozi hao kuwa hakuna sababu ya vibanda hivyo kuendelea kubaki mahala hapo pakiwa patupu.

Alisema wafanyabiashara wengi wameshahama wenyewe katika eneo hilo na kurudi katika masoko na maeneo mengine ya mjini na kutaka vibanda vilivyopo viondolewe.

Akikagua maeneo mengine wakati wa ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa alizitaka taasisi hizo pia kuhakikisha wanabomoa vibanda vyote vya biashara vilivyojengwa katika maeneo ya hifadhi ya barabara pamoja na kuondoa mabango ya biashara yaliyochakaa katika maeneo hayo.

Alisema vibanda hivyo vimejengwa kinyume na sheria, lakini vimekuwa vikiufanya mji kuonekana mchafu na mandhari yasiyovutia. Aliyataka mabaraza ya manispaa katika mkoa huo, kudhibiti wafanyakazi wao wanaohusika na makusanyo ya kodi na kwa kuwa bado kuna uvujaji wa mapato katika taasisi zao.

"Bado sijaridhika na utendaji wa ukusanyaji wa mapato katika taasisi hizo hasa za maegesho ya gari," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Zanzibar, Ali Khamis Juma, alimhakikishia mkuu huyo kuwa agizo lake litatekelezwa kwa muda uliopangwa. Naye Mstahiki Meya wa jiji hilo, Saleh Juma Kinana, alisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wafanyabiashara ili kuondoa tatizo baadaye.

Ziara hiyo ilihusisha maeneo ya Kariakoo, Kijangwani, Michenzani, Darajani, mnada wa samaki Bwawani, Saateni na maeneo mengine ya Wilaya ya Magharibi B Unguja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**AISHA FUAD ABDALLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4555-0001** kilichotolewa na **GLORIOUS ACADEMY** mwaka **2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: MAL/RB/4521/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GOODLUCK ARISTARICK KIMARIO** amepotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0506/0092** kilichotolewa na shule ya secondary UNGWASI mwaka **2017** yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa: DAR/MBURB/802661/2020**

116002902

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**GEORGE LUGENDO KISOMBA.** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji aina ya **Piaggio APE** yenye namba za usajili **MC 654 AYM.** Chassis No. MBX0002CFSE892459,Engine No. TBPIMD53014879.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/80203/2020.**

116003402

## KADI YA GARI IMEPOTEA

Ndugu **EMMANUEL WASTON MWATIYA** anatangaza kupotelewa na na kadi ya gari kama ifuatavyo:

**Aina ya gari : Land Cruiser GX yenye namba za usajili T 771 BMQ**

Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

**POLICE LOSS REPORT NAMBA: MBE/MBE/RB/804261/2020**

116003702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**
**SHAURI NA. 227 LA 2020**

**HERMAN J. MANUMBU................................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**AMINA K. KASWALA.................................MDAIWA**

**KWA : AMINA K. KASWALA**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua Shauri / Ombi dhidi yako katika baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 03/12/2020 katika Chumba cha Baraza, Barabara ya Posta. Jengo liko Mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo. \imetolewa name kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 13/11/2020.

116003202

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**Lydia John Mhina** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **AB 531777** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **12/7/2012.** Muda wa kuisha matumizi ni tarehe 11/7/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/CHU/RB/790278/2020.**

116002402

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ELIBARIKI E. NNKO** anatangaza kupotea kwa Result Slip yenye index namba **S.0647/0081** iliyotolewa na **NGARENANYUKI SEKONDARI** mwaka **2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: ARU/ARU/RB/789029/2020.**

116002302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5**
**KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;339/2020

Ombi la STUMAI HAMIS KAZILI ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI RASHIDI ALLY.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/11/2020.

116002602

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na...82 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU BAHADURSINH HIRJI SAMPAT**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**MRS BHARTI BAHADURSINH**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa December 2020.

NAIBU MSAJILI

116002702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**OMARI RAMADHANI MHANDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 758 BFH.** Chassis **NoLBRSPJB51H9006346.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/6088/2020.**

116002802

## KUPOTEA KWA CHETI



**RHODA KAHUMBA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0358/0043** kilichotolewa mwaka **1992** na shule ya secondary **SHIGHATINI** ,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa SBR/IR/RB/2107/2014**

116001802

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL A. CHEZUE**

Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 3674/0046 kilichotolewa na shule ya secondary **ST.JOSEPH MILLENIUM** yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa
**DAR/MSI/RB/798123/2020**

116003602

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Wanajeshi kutoka vikosi vya serikali ya Ethiopia wakiwa mjini Tigray, tayari kwa makabiliano na vikosi vya mji huo. **PICHA: DW**

# Operesheni za kijeshi Tigray zafikia tamati

**ADDISABABA,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amesema operesheni za kijeshi jimboni Tigray zitaingia katika awamu ya mwisho, wakati ambapo shinikizo la kimataifa linaongezeka dhidi yake la kuumaliza kwa amani mzozo huo.

Juzi, kulifanyika mashambulizi mapya ya anga katika Mji Mkuu wa jimbo hilo, Mekele, wakati wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakitoa wito wa kumalizwa kwa mzozo huo na kufanyika mazungumzo.

Abiy, ambaye ni mshindi wa tuzo ya kimataifa ya Amani ya Nobel mwaka jana, alitangaza kampeni ya kijeshi katika jimbo hilo pinzani Novemba 4, akisema ilisababishwa na mashambulizi yaliyofanywa na Chama cha Tigray Peoples Liberation (TPLF) kilichopo mjini Tigray, kwenye makambi ya kijeshi ya serikali.

Mapigano hayo yamesababisha vifo vya mamia ya raia na wengine 25,000 wakikimbilia nchi jirani ya Sudan, ambako kunatarajiwa wakimbizi wengi huenda wakaingia nchini humo.

Jana, Waziri Mkuu Abiy aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter kwamba: "Muda umekwisha na kufafanua kuwa muda wa siku tatu uliotolewa kwa vikosi maalumu vya Tigray pamoja na wanamgambo ili kujisalimisha kwa vikosi vya serikali badala ya kuendelea kuwa vibaraka wa utawala haramu wa kijeshi umekamilika". **DW**

# Marekani kuondoa wanajeshi zaidi Afghanistan, Iraq

**WASHINGTON,** Marekani

MAOFISA katika serikali ya Marekani wamesema kwamba Rais Donald Trump anatarajia kupunguza idadi ya wanajeshi wa Marekani nchini Afghanistan kwa zaidi ya nusu.

Wamesema katika mkakati huo, Rais Trump anatarajia kubakisha wanajeshi 2,500 nchini humo, ifikapo Januari 15.

Kulingana na Shirika la Habari la Associated press, amri hiyo ya Rais Trump hata hivyo haitatimiza ahadi yake ya kuondoa kabisa wanajeshi wa Marekani nchini Afghanistan ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Hata hivyo, Hatua hiyo ilipingwa na washauri wa kijeshi na kidiplomasia. Pentagon inatarajiwa pia kupunguza wanajeshi wa Marekani nchini Iraq kufikia 2,500, ikiwa ni punguzo la zaidi ya wanajeshi 500.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Rais Trump kuwafuta kazi maofisa wa ngazi ya juu Wizara ya Ulinzi na kuteua wale wanaounga mkono maamuzi yake.

Maofisa wa serikali walisema kwamba viongozi wa jeshi waliarifiwa wikendi iliyopita kuhusu mpango huo.

Akizungumza mwanzoni mwa wiki bungeni, Seneta wa Kentucky alisema: "Tumekuwa tukipunguza idadi ya wanajeshi lakini kazi muhimu ya kulinda usalama wa taifa la Marekani na maslahi ya Wamarekani".

Rais Trump kwa muda mrefu ameyataka majeshi ya Marekani kurejea nyumbani na amekuwa akikosoa operesheni za kijeshi kuwa yamekuwa yakigharimu na kukosa ufanisi. **DW**

# WHO yazindua mkakati mapambano saratani

**WHO**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limezindua mkakati mpya wa kupambana na kuiangamiza saratani ya kizazi, kwa matumizi mapana ya chanjo, vipimo vipya na matibabu ili kuokoa maisha ya watu kufikia mwaka 2050.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, awali ilikuwa kama ndoto kupambana na kuondoa kabisa aina yoyote ya saratani, lakini sasa shirika hilo limejihami na zana za gharama nafuu na za kutosha kukabiliana na Saratani.

Mkatati huo umetoa wito kwa mataifa mbalimbali kutoa chanjo ya saratani ya kizazi, angalau kwa asilimia 90 ya wasichana walio chini ya umri wa miaka 15, ifikapo mwaka 2030.

Aidha WHO katika mkakati wake mpya imetoa wito kwa angalau asilimia 70 ya wanawake kuhakikisha wanapimwa saratani ya kizazi, wanapofikisha umri wa miaka 35, kisha kupima tena wanapofikia umri wa miaka 45.

**Ugonjwa wa Corona umevuruga mpangilio wa chanjo, upimaji na matibabu ya saratani ya kizazi na kufungwa kwa mipaka katika mataifa mbalimbali kumepunguza upatikanaji wa dawa.**

Alisema asilimia 90 ya waliopatikana na ugonjwa huo wanapokea matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na WHO, zaidi ya wanawake nusu milioni duniani wanapimwa na kupatikana na saratani kila mwaka, huku mamia kati yao wakifariki kutokana na ugonjwa huo.

Pia imeeleza kuwa iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa idadi itaendelea kuongezeka.

Wiki iliyopita, WHO katika mkutano wake wa kila mwaka unaowajumuisha wanachama wake kutoka mataifa 194 walikubaliana kubuni mbinu za kuangamiza saratani.

Mkurugenzi msaidizi wa WHO, Princess Nothemba Simelele, alisema wamepiga hatua kubwa na kwa mara ya kwanza dunia imekubaliana kuitokomeza saratani ambayo inaweza kuepukika kwa kutumia chanjo, pia inaweza kutibika iwapo itagunduliwa mapema.

Hata hivyo, WHO imesema kuna mipango mizuri ya kurahisisha upimaji, kupunguza gharama na upatikanaji wa matibabu licha ya mkakati huu mpya kuzinduliwa wakati ulimwengu umejikita katika kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Simelele alisema ugonjwa wa Corona umevuruga mpangilio wa chanjo, upimaji na matibabu ya saratani ya kizazi na kufungwa kwa mipaka katika mataifa mbalimbali kumepunguza upatikanaji wa dawa.

Aidha, alisema kutoa chanjo kwa wasichana tisa kati ya 10 walio chini ya umri wa miaka 15, kuboresha upimaji na matibabu kwa wanaogua, kunaweza kupunguza athari ya saratani ya kizazi kwa asilimia 40 na kuzuia vifo vya takribani wanawake milioni tano ifikapo mwaka 2050. **DW**



# POGBA AAMBIWA ARUDI JUVE

**TURIN,** Italia

KIUNGO wa zamani wa Juventus, Claudio Marchisio, amemwambia nyota wa Manchester United, Paul Pogba, arudi kwa miamba hao wa Serie A ili "kuwa na furaha tena ".

Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoa United, ambako alirudi kutoka Juve mwaka 2016.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ameibua uvumi kuhusu majaliwa yake wakati alipobainisha kutokuwa na furaha wakati akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa, akisema "kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa navuta hewa safi".

Pogba ameripotiwa kwamba anawaniwa na Juventus na miamba wa LaLiga, Real Madrid, na mchezaji mwenzake wa zamani, Marchisio angependa kumuona akirudi Turin.

Aliandika kwenye ukurasa wa twitter kuhusu Pogba: "Tafadhali @paulpogba. "Njoo @juventusfc... utakuwa na furaha tena. Na mimi pia."

Pogba alitumia misimu minne akiwa Juventus kati ya mwaka 2012 na 2016, akishinda taji la Serie A mara zote kwa kipindi hicho, huku pia akishinda Coppa Italia na Supercoppa Italiana.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018, ameshinda Kombe la EFL na Europa tangu aliporudi United.

Pogba amecheza mechi saba za Ligi Kuu England msimu huu, huku vijana hao wa Ole Gunnar Solskjaer wakiwa nafasi ya 14 kwenye msimamo.

United watarudi kwenye Ligi Kuu Jumamosi watakapocheza na West Brom.



# Ramos: Sitaacha kupiga penalti

**SEVILLE,** Hispania

SERGIO Ramos hana mpango wa kuachana na jukumu la kupiga penalti kwa timu ya Taifa ya Hispania, licha ya kukosa mbili dhidi ya Uswisi.

Ramos alifikisha mechi 177 za kimataifa, na kuizima rekodi ya Gianluigi Buffon wa Italia kwa kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi timu ya taifa kwa bara la Ulaya, lakini alikosa penalti mbili wakati wakitoka sare ya bao 1-1 kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA, Jumamosi.

Mlinzi huyo hadi sasa ameifungia Hispania na Real Madrid penalti 25 kabla ya kukosa hizo mbili.

Ramos, amesema ataendelea na majukumu yake ya kupiga penalti kama kawaida.

"Kungekuwa na penlati nyingine, bila shaka yoyote ningepiga na nitaendelea kufanya hivyo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Hispania jana Jumanne ilicheza na Ujerumani mjini Seville, kwenye mchezo wa Kundi A4 wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Ramos mwenye umri wa miaka 34, amesema alikuwa na rufaha kubwa kufikia rekodi ya kucheza mechi nyingi za kimataifa na hakuwa tayari kuzungumzia kuhusu kutundika daruga.

# Elneny wa Arsenal akutwa na corona

**CAIRO,** Misri

KIUNGO wa Arsenal raia wa Misri, Mohamed Elneny amekuwa mchezaji wa hivi karibuni zaidi kwenye Ligi Kuu England kukutwa na virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Taarifa ya timu ya Taifa ya Misri, ilisema kupitia kwenye tovuti yake Jumatatu kwamba, Elneny amekutwa na virusi hivyo kabla ya mchezo wa jana Jumanne dhidi ya Togo wa kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), lakini hajaonyesha dalili zozote na amejitenga.

Elneny, ambaye alichezea wakati Misri ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Togo Jumamosi, pia ataukosa mchezo wa Ligi Kuu ya England wa Arsenal dhidi ya Leeds United, Jumamosi.

Mchezaji mwenzake wa timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, pia alikutwa na COVID-19 Ijumaa na hatakuwapo kwenye mchezo wa Liverpool wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Leicester City mwishoni mwa wiki.

Misri ipo nafasi ya pili kwenye Kundi lake la G ikiwa na pointi tano kutokana na mechi tatu, ikipitwa pointi tatu na vinara Comoros, ambao wamecheza mchezo mmoja zaidi, mbili zaidi ya Kenya na nne dhidi ya Togo, ambao pia wana mchezo mkononi.

Timu mbili za juu zinafuzu kucheza michuano ya mashindano hayo.



# Giroud atakiwa kuondoka Chelsea

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amemwambia, Olivier Giroud lazima "atafute sehemu nyingine" kabla ya mapumziko yajayo ya mechi za kimataifa, baada ya kuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza pale Chelsea.

Giroud amefunga mabao 42 katika mechi 102 za Ufaransa, yakimfanya kushinda nafasi ya pili kwa kuwa mfungaji wa wakati wote wa Ufaransa nyuma ya Thierry Henry.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ameendelea kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha Deschamps na pia jana Jumanne alitarajiwa kucheza kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Sweden.

Hata hivyo, amekuwa hapati nafasi ya kucheza pale Chelsea msimu huu, akianza katika mechi moja tu kwa Blues hao katika mashindano yote, na Deschamps amemshauri Giroud kutafuta namna nyingine.

"Olivier Giroud anajua hilo, hali ya leo haiwezi kumwendesha milele. Kabla ya Machi anatakiwa kutafuta sehemu nyingine," alisema Deschamps – kiungo wa zamani wa Chelsea akiiambia radio ya Ufaransa, RTL.

"Kamwe huwa sitoi ushauri, natoa mawazo yangu. Na mwisho wa siku, ni maamuzi ya mchezaji mwenyewe. Yupo kwenye hali ambayo mara zote inamuweka kwenye nafasi ngumu.





# MGOMBEA URAIS BARCA HAMTAKI TENA NEYMAR

**BARCELONA,** Hispania

MGOMBEA urais wa Barcelona, Victor Font, hana mpango wa kumsajili tena Neymar kutoka Paris Saint-Germain kama atashinda uchaguzi huo.

Neymar alishinda mataji manne akiwa pale Camp Nou kabla ya kujiunga na miamba hao wa Ufaransa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222, Agosti 2017.

Huku kukiwa na uvumi wa kumhusisha Neymar kurudi pale Catalunya, Font ameondoa uwezekano wa kumsajili tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Kikatiba, Neymar hayupo kwenye mipango yangu," alisema Font, ambaye awali alibaainisha mpango wa kutaka kumrudisha Pep Guardiola pale Catalunya kuungana na Lionel Messi.

"Kwa sababu ya kifedha na nyinginezo, kama kesi aliyofungua ya madai dhidi ya klabu na ukweli ni kwamba aliondoka klabuni kwa hali ambayo si nzuri kabla ya kuanza kwa msimu mwaka 2017."

Neymar amefunga mabao 49 katika mechi 56 za Ligue 1 tangu alipotua hapo PSG na ametoa pasi za mwisho 29.

Kwa kipindi alichocheza Barca, amehusika moja kwa moja na mabao 164 katika mechi 186, akiisaidia klabu hiyo kushinda mataji nane.

Font anapewa nafasi kubwa ya kushinda nafasi ya urais kwa klabu hiyo katika uchaguzi utakaofanyika Januari 24, mwakani.

# *Suarez kuikosa Barcelona LaLiga*

**MADRID,** Hispania

LUIS Suarez amekutwa na virusi vya corona na ataukosa mchezo wa Atletico Madrid wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya timu yake ya zamani, Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, pia aliukosa mchezo wa jana Jumanne wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Brazil.

Shirikisho la Soka la Uruguay lilithibitisha Jumatatu kwamba, Suarez na mchezaji mwenzake, Rodrigo Munoz pamoja na mmoja wa maofisa wa benchi la ufundi, Matias Faral, kwa sasa wamejitenga kwa siku 14 baada ya kukutwa na maambuziki ya corona.

Habari hizo zimekuja siku tano kabla ya Suarez kuivaa Barcelona, klabu ambayo aliondoka Septemba baada ya miaka sita pale Camp Nou.

Amecheza mechi tisa kwa Atletico tangu alipojiunga na amefunga mabao matano kwenye mechi sita za LaLiga.

Ni Mikel Oyarzabal pekee wa Real Sociedad ndiye amefunga mabao mengi, akiwa amecheza me



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG ABWATUKA CAF KUGEUZWA MATEKA

●●● Ni kwa kulazwa uwanja wa ndege Gambia, asema inatakiwa kuwajibika kwa hilo ili soka la...

**BANJUL,** Gambia

PIERRE-Emerick Aubameyang amelihoji Shirikisho la Soka la Afrika (CAF), baada ya kikosi cha Gabon kuwekwa kama "mateka" kwa muda wa saa sita katika uwanja wa ndege wa Gambia, kabla ya mchezo wao wa kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika, AFCON 2022.

Straika huyo wa Arsenal, Aubameyang alionyesha mkanganyiko huo kwa kuposti video kwenye ukurasa wake wa Instagram mapema asubuhi ya Jumatatu, akiwaonyesha wachezaji wenzake wakiwa wamelala sakafuni baada ya kunyang'anywa hati zao za kusafiria na maofisa wa usalama.

Lakini saa zilivyozidi kwenda, aliposti picha nyingine za wachezaji hao wakiwa wamelala sakafuni, huku mizigo yao wakiifanya kama mito ya kulalia.

**Wakiwa wamewasili majira ya saa 5:30 usiku kwa saa za Gambia, Aubameyang alionekama kupagawa baada ya kusubiri kwa saa tatu, na saa 8:31 usiku akaandika kwenye ukurasa wake wa mtandao huo wa kijamii: "Bado tunasubiria kuingia Gambia, na tunacheza saa 10 jioni. Vizuri."**

Baadaye alionyesha video ya wachezaji wenzake wakitania na kusikiliza muziki, huku Aubameyang akiandika tena "hatukatishwi tamaa".

Saa 12:00 alfajiri kikosi cha Gabon kiliruhusiwa kuingia nchini humo, ikiwa ni saa 10 kabla ya mchezo wao.

"Hatimaye tupo kwenye basi. Asante kwa morali zaidi, Gambia," aliandika Aubameyang.

Lakini wakati Aubameyang akitoa posti hizo, ukaibuka mjadala mkubwa kwenye ukurasa wa twitter kuishutumu CAF na Gambia.

Mashabiki wengi wa soka waliishutumu CAF kwa kushindwa kuchukua hatua za haraka, huku Aubameyang akiinyooshea kidole CAF moja kwa moja.

"Hili halitatukatisha tamaa sisi," alisema.

"CAF inatakiwa kuwajibika kwa hili, tunataka soka la Afrika likue, lakini CAF inaonekana kuwa kikwazo namba moja.

## ZISIKUPITE

### SANCHO BADO LULU UTD

MANCHESTER United bado wanamtaka winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, na wanajaribu kutaka kupata saini yake kabla ya mashindano ya euro mwakani. ***(90 min)***

### PSG WAMTAKA RAMOS

KLABU ya Paris St-Germain imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Real Madrid na Hispania, Sergio Ramos, mwenye umri wa miaka 34. ***(AS)***

### MBAPPE, NEYMAR KUFUNGWA

PSG pia wanajaribu kutaka kuwafunga zaidi kwa kuwaongeza mikataba, Mfaransa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21 na mshambuliaji Mbrazil Neymar mwenye umri wa miaka 28. ***(Goal)***

### EVERTON, SPURS KWA MILIK

EVERTON na Tottenham Hotspur kwa pamoja zipo katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Arkadiusz Milik raia wa Poland mwenye umri wa miaka 26, ambaye ada yake inatajwa kuwa pauni milioni 10. ***(Sun)***

### CELTIC WAMTAKA HENDERSON

KLABU ya Celtic inataka kumsajili golikipa wa Manchester United na England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 23, kwa mkataba wa mkopo, wakati wa dirisha la Januari. ***(90 min)***

### BARCA WAMWANIA MUSTAFI

KLABU ya Barcelona inaangalia uwezekano wa kumchukua beki wa Arsenal na Ujerumani, Shkodran Mustafi mwenye umri wa miaka 28.

### TRAORE ATOA NENO WOLVES

STRAIKA wa Wolves na Hispania, Adama Traore, mwenye umri wa miaka 24, anaamini kuwa hajakubaliwa kuanza kucheza mechi kwa sababu amekataa kurefusha mkataba wake klabuni hapo. Mkataba wake wa sasa unaendelea hadi 2023. ***(The Athletic)***

### TERRY ANUKIA DERBY

MLINZI wa zamani wa Chelsea na England, John Terry mwenye umri wa miaka 39, ni mmoja wa watu wanaoweza kuchukua kazi mpya ya ukocha katika timu ya Derby County. ***(Mail)***

### LEICESTER KUMFUNGA EVANS

KLABU ya Leicester City imeanza mazungumzo na beki wa Ireland Kaskazini, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 32, kuhusu mkataba mpya. ***(The Athletic)***

### BARCA KUUZA NYOTA WA4

BARCELONA wako tayari kuwauza wachezaji wanne Januari - Junior Firpo mwenye umri wa miaka 24, Samuel Umtiti (26), Matheus Fernandes (22), na kiungo wa mshambulizi Mdenmark, Martin Braithwaite, 29. ***(Sport)***

### UTD YATAJWA KWA CARMO

KLABU ya Manchester United imekuwa ikihusishwa na mlinzi wa Sporting Braga, Mreno David Carmo mwenye umri wa miaka 20. ***(The Athletic - subscription required)***

## HABARI MICHEZO

# DUBE WA AZAM AITUNGUA ALGERIA IKIWA NA MAHREZ

**Na Mwandishi Wetu**

KINARA wa mabao Ligi Kuu Bara, Prince Dube, anayeichezea Azam FC, ameendeleza moto wake wa kucheka na nyavu baada ya kuiokoa Zimbabwe kulala nyumbani dhidi ya mabingwa watetezi wa michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), Algeria.

Dube ambaye hadi sasa yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Bara sambamba na Adam Adam wa JKT Tanzania, kila mmoja akiwa na mabao sita, juzi aliiokoa timu yake ya taifa kwa kufunga bao la kusawazisha wakati wakilazimisha sare ya mabao 2-2 katika mechi hiyo ya Kundi H kuwania kufuzu Afcon 2022 iliyopigwa Harare, Zimbabwe.

Katika orodha hiyo ya wafungaji wa Ligi Kuu, Dube na Adam wanafuatiwa kwa karibu na John Bocco, Meddie Kagere (Simba), Abraham Meshack (Gwambina), Obrey Chirwa (Azam), Yusuph Mhilu (Kagera Sugar) na Bigrimana Blaise wa Namungo, ambao kila mmoja amecheka na nyavu mara nne.

**Kwa upande wa mchezo wao wa juzi kuwania kufuzu Afcon nchini Cameroon 2022, Andy Delort na Riyad Mahrez waliwatanguliza mbele 'Mbweha wa Jangwani' hao ('Desert Foxes') kwa mabao ya mapema, kabla ya Knowledge Musona na Dube kuisawazishia Zimbabwe.**

Matokeo hayo yanaifanya Algeria kufikisha pointi 10, wakati Zimbabwe inabaki nafasi ya pili na pointi zake tano, moja mbele ya Botswana, huku Zambia ya kiungo wa Simba, Clatous Chama, ikiburuza mkia na alama zake tatu, wakati huu kila timu ikiwa imebakiza mechi mbili.

Katika kundi hilo, Botswana ikiwa nyumbani, iliichapa Zambia kwa bao 1-0, matokeo ambayo yanazidi kulifanya Kundi H liwe gumu.

Kwingineko, Malawi ikiwa nyumbani ililazimishwa sare tasa na Burkina Faso huku Sudan Kusini ikishinda 1-0 dhidi ya Uganda iliyokuwa ugenini, wakati Sao Tome and Principe ikikubali kipigo cha mabao 4-2 kutoka kwa wageni wao, Afrika Kusini.

Eswatini ilikubali kulazimishwa sare tasa nyumbani dhidi ya Congo, huku Msumbiji ya kiungo wa Simba, Luis Miquissone ikichapwa mabao 2-0 kwao dhidi ya Cameroon, wakati Gambia yenyewe ilishinda 2-1 nyumbani dhidi ya Gabon.

## TOKOMEZA KISUKARI...



Wananchi mbalimbali wakifanya mazoezi wakati wa Siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Ugonjwa wa Kisukari, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga sasa yamalizana na Zahera*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imefanikiwa kumlipa stahiki zake zote zilizokuwa kwenye mtakaba, Kocha Mkuu wao wa zamani, Mwinyi Zahera.

Kocha huyo amethibitisha kumalizana na Yanga na kueleza sasa hadai kitu, ingawa amesema kuwa kulikuwa na pesa ambazo alikuwa ametoa nje ya mkataba ambazo yeye amezisamehe kutokana na kutokuwa ndani ya mkataba na amefanya hivyo kutokana na moyo wake wa kujitolea, huku akiwa na mapenzi na klabu hiyo.

"Ni kweli tumemaliza na Yanga, sidai kitu, stahiki zangu zote ambazo zilikuwa kwenye maandishi ndani ya mkataba nimelipwa. Kulikuwa na pesa zingine ambazo nilikuwa natoa nje ya mkataba, kwa sababu haziko kwenye maandishi mimi siwezi kudai, ni kwamba nilitoa kwa mapenzi yangu kwa klabu ambayo naipenda," alisema Zahera ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu ya Gwambina iliyopo Misungwi jijini Mwanza.

Zahera hakutaja kiasi cha pesa alizolipwa, lakini alisema pesa zote alizozipata amezipeleka kwenye vituo kadhaa vya soka vya kulelea vijana 'academy', vilivyopo hapa nchini.

"Sijatumia hata senti moja, zote zimezipeleka zikasaidia soka la vijana hapa nchini, ni mchango wangu kwa ajili ya kuinua soka la Tanzania," alisema.

Alipoulizwa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kama yeye mwenyewe ameongea na kuthibitisha kuwa amelipwa, basi wao hawana tatizo.

"Kwanza kabisa nikwambie tu kuwa mimi niko likizo kwa sasa, sijapata taarifa za kutosha sana kuhusu suala hilo, nadhani nitakapowasiliana na viongozi wangu nitakuwa na maelezo ya kutosha kuhusu suala hilo hapo siku za usoni, lakini kama yeye mwenyewe ameshasema na kuthibitisha kwamba amelipwa na haidai tena Yanga, basi hakuna tatizo," alisema Bumbuli.

Zahera raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alihudumu ndani klabu hiyo kwa mwaka mmoja, huku akiwa amesaini mkataba wa miaka mwili.

Alijiunga na klabu hiyo katikati ya Machi 2018 na kutimuliwa mwanzoni mwa Novemba mwaka jana, baada ya matokeo mabaya ya timu hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara, nafasi yake ikichukuliwa na Luc Eymael ambaye naye alitimuliwa na mikoba yake kuchukuliwa na Zlatko Krmpotic kabla naye kutimuliwa na Mrundi Cedrick Kaze kupewa mikoba.

## Mfaume ampania Mmalawi ulingoni

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA pambano lake la kimataifa dhidi ya bondia Mmalawi Stone Makani, bingwa wa masumbwi Afrika Mashariki na Kati, Mfaume Mfaume (pichani chini) anayepigana uzito wa kilo 69 (super weight), amesema anafanya mazoezi magumu kujiandaa kupanda ulingoni Desemba 26, mwaka huu.

Akizungumzia pambano hilo, alisema amejipanga vizuri na kuwataka mapromota wa mchezo huo wawe wanawaletea mabondia ambao wapo juu kiuwezo ulingoni.

"Naendelea na mazoezi kujiandaa na pambano hilo, ninaomba Watanzania waje kuniunga mkono siku ya pambano hilo ikifika," alisema Mfaume.

Alisema hapendi kupigana mara kwa mara kwa sababu ya kujiepusha kuumia vibaya wakati pambano lenyewe hapati pesa nyingi zaidi ya kuumia.

Mfaume aliwataka mabondia wenzake watumie akili pamoja na nguvu nyingi wanapokuwa ulingoni ili kutompa nafasi mpinzani.

Aidha, Mfaume ambaye hadi sasa ameshacheza mapambano 26 nje na ndani ya Tanzania, alisema yupo tayari kupigana na bondia yeyote ambaye atahitaji kupanda ulingoni naye kutokana na kuwa na uwezo mzuri.



## Tenesi kwa wenye ulemavu Nov. 28

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wenye ulemavu ya mchezo wa tenesi kwa vijana wenye umri wa miaka 18, yanatarajiwa kuanza kurindima katika Klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam kuanzia Novemba 28-29, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Makocha wa mchezo huo ( TTCA), Kevin Kipingu, alisema mashindano hayo pia yatashirikisha wa wachezaji ambao hawana ulemavu.

Alisema mikoa ambayo itashiriki mashindano hayo ni Simiyu, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Pwani pamoja na wenyeji, Dar es Salaam.

"Mshindi atakayepatikana kwenye mashindano hayo atapata zawadi ya kikombe," alisema Kipingu.

Alisema mashindano hayo yatachezeshwa na marefarii wawili ambapo kwa upande wa wasiokuwa na ulemavu watachezeshwa na Salum Mvita wakati wengine wakichezeshwa na Riziki Salum.

Alisema mtanange huo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kupata wachezaji watakaounda timu ya taifa.

# Michezo

Jumatano Novemba 18, 2020

Nipashe



Aubameyang abwatuka CAF kugeuzwa mateka UKURASA 22

NDIO ZANGU...



Kiungo nyota wa Simba, Mzambia Clatous Chama, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa African Sports ya Tanga katika mchezo wa kirafiki ulipigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam juzi usiku na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Mastraika wa Plateau waitisha Simba CAF

●●● Sven anasa mikanda ya video, asema wana kasi na hutumia nguvu, ageukia mabeki, huku...

**Na Saada Akida**

HUKU akiendelea kukisuka kikosi chake kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali kusaka nafasi ya kuingia hatua ya makundi, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, imembidi kuelekeza nguvu zaidi katika safu yake ya ulinzi baada ya kunasa mikanda ya video ya wapinzani wao, Plateau United ya Nigeria, ameeleza.

**Hatua hiyo imetokana na kubaini ubora wa safu ya ushambuliaji ya Plateau, kutokana na washambuliaji wake kuwa na kasi wanapounasa mpira huku wakicheza kwa kutumia nguvu zaidi.**

Safu ya ulinzi ya Simba, inayoundwa na Muivory Coast, Pasca Wawa, Mkenya Joash Onyango na mabeki wa pembeni Mohamed Hussein 'Tshabalala' pamoja na Shomary Kapombe, imekuwa ikilaumiwa kutokana na kuwa wepesi wa kugeuzwa na washambuliaji kirahisi huku udhaifu wao mkubwa ukiwa ni kukosa kasi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya African Sport, uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Sven alisema amefanikiwa kupata video za michezo ya nyuma ya Plateau United na kubaini ni timu nzuri na ina washambuliaji wenye nguvu.

Alisema wapinzani wao wana timu nzuri yenye washambuliaji wenye nguvu na kasi wakiwa na mpira, hali ambayo ameanza kuifanyia kazi kuhakikisha anawapa majukumu muhimu safu yake ya ulinzi kuwa imara zaidi.

"Wana washambuliaji wenye kasi, pia hata safu yao ya ulinzi ipo imara, nimepanga kuhakikisha naongeza mbinu kwa mabeki na washambuliaji wangu kuhakikisha tunapata matokeo chanya mbele ya wapinzani wetu hao," alisema Sven.

Alisema wanahitaji kufanya maandalizi kwa umakini mkubwa na kufanyia kazi kikosi chake katika kila idara baada ya kuona ubora wa Plateau United.

"Malengo yetu ni kusonga mbele, tunalazimika kufanya maandalizi ya kutosha kwa kuboresha kikosi changu kila idara kwa kuwapa mbinu kulingana na jinsi nilivyoziona video za mechi za nyuma walizocheza wapinzani wetu," alisema Sven.

Aidha, alisema ana kazi kubwa ya kufanya kwa kipindi hiki kuhakikisha anaimarisha kikosi chake hasusan safu ya ulinzi, lakini viungo wakabaji, huku akihakikisha washambuliaji wote wanakuwa imara kukabiliana na Wanigeria hao.

Simba ambayo katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), itaanzia ugenini Nigeria, mchezo ukipigwa kati ya Novemba 27-29 kabla ya kurudiana kati ya Desemba 4-6, mwaka huu, juzi usiku iliicheza mechi ya kirafiki dhidi ya African Sport ya Tanga na kulazimishwa sare tasa.

Mechi hiyo, mbali ya Sven kuitumia kuwajengea wachezaji wake utimamu wa kimwili ambao hawapo na timu zao za taifa, pia ulikuwa maalum kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union itakayopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Jumamosi wiki hii kabla ya kukwea pipa kuelekea Nigeria.

## ZFF sasa yaziachia klabu 'zigo' la kulipa marefa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefanya marekebisho katika baadhi ya kanuni zake za uendeshaji wa ligi, ambapo kuanzia msimu huu timu mwenyeji ndio itakayowajibika kuwalipa marefa.

Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohmed Ameir, amesema katika msimu huu wa 2020-21 mapato ya mlangoni yatakayopatikana kwa upande wa Klabu za Ligi Daraja la Kwanza Kanda yatakatwa gharama za kuwalipa waamuzi.

Akitolea ufafanuzi kuhusu hatua hiyo, alisema msimu huu timu mwenyeji itachukuwa mapato yote ya mlangoni, hivyo itatoa gharama za malipo ya waamuzi, hiyo ikiwa ni tofauti na msimu uliopita ambapo ZFF ilikuwa ikibeba jukumu hilo la kuwalipa.

Alisema uamuzi huo umekubaliwa na kupitishwa katika kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Mashindano na Klabu za Kanda ya Unguja, lengo likiwa ni kuepusha malimbikizo ya madeni kwa waamuzi yanayojitokeza kila msimu.

"Timu itakayocheza uwanja wa nyumbani mapato yote yatakuwa yake, hivyo hakutakuwa na asilimia ya ZFF kama tulivyozoea, bali sasa kutakuwa na asilimia ya waamuzi, hivyo timu kabla ya kutoa kitu chochote kwa mujibu wa fomu ya mgao wa mapato uwanjani, kwanza itatakiwa kutoa asilimia ya waamuzi," alifafanua.

Aidha, alisema ZFF itafuatilia kwa karibu mechi zote ili kuepusha vitendo vya rushwa baina ya waamuzi na klabu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >